# Pambazuko

Toleo Namba 151 | Jumatatu, Januari 19-25, 2026


# Mabilioni kutumika 'kusafisha nyota' ya Tanzania

Uk. 6&7

- Ni kandarasi ya kulipa shilingi bilioni 2 kwa kampuni ya Marekani




# Kiini macho Sheria ya Manunuzi

Uk. 9

- Ni asilimia mbili tu inayotekelezwa badala ya 30

## Mfanyabiashara avuruga Jiji Dar es Salaam

Habari Uk. 12

## Tahariri

# Karibu Makonda, huku kunaponya taifa

RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, amefanya mabadiliko ya baadhi ya wasaidizi wake wakuu kwenye baraza la mawaziri.

Katika mabadiliko hayo, Rais Samia amemteua Mbunge wa Arusha Mjini, Paul Christian Makonda kuwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, akichukua nafasi ya mtangulizi wake, Profesa Palamagamba Mwaluko Kabudi. Profesa Kabudi ametangazwa kuwa msaidizi wa Rais – Kazi Maalum.

Hakika ni kwamba mabadiliko hayo yamechukuliwa na Rais Samia akiamini kuwa Makonda atamsaidia zaidi kwenye eneo hilo linalobeba alama kubwa za utambulisho wa taifa, staha za Watanzania na zaidi sana demokrasia.

Katika kuilea demokrasia kuu; ya kuruhusu vyombo vya habari kufanya kazi kwa uhuru na weledi na Watanzania kuzungumza kwa uwazi, Pambazuko linaamini kuwa Rais Samia amemuweka Makonda ili kulinda na kuondoa vizingiti vya vyombo vya habari hivyo kufanya kazi zake bila woga wala inda.

Kwamba sasa chini ya Makonda, bila kujali historia yake huko nyuma, vyombo vya habari visitingwe wala kutishwa ama kujitisha vyenyewe kwenye utendaji wake. Viwe huru na kutumia haki kuhabarisha umma na dunia.

Kwamba sasa vyombo vikomae kusaidia uongozi wa Rais Samia na Tanzania kuibua “madudu,” hasa ya rushwa, utendaji mbovu wa baadhi ya watumishi wasiokuwa waaminifu ili kujenga Tanzania tunayoitamani kila uchao.

Kwamba vyombo vya habari visione haya kuanika wanaokwamisha ustawi na neema ya Mtanzania kwa kuminya haki zao.

Pambazuko linabeba imani kwamba uteuzi wa Makonda kwenye wizara hii nyeti, ni utashi wa Rais Samia kutaka kuponya majeraha na madhila yaliyotokea Oktoba 29, mwaka jana – 2025, wakati na siku chache baada ya kufanyika kwa uchaguzi mkuu. Katika kipindi hicho, historia mbaya iliandikwa Tanzania – kwa baadhi ya watu kuuawa na mali kuharibiwa.

Tukiacha eneo la habari, Pambazuko linaamini pasinashaka kuwa Makonda anakwenda kuamsha ari ya Watanzania kupenda utamaduni na sanaa zao, kwamba kupitia maeneo hayo, waziri huyo mpya anapanga kuondoa “udumavu na dharau” kwenye asili yetu.

Katika miaka ya hivi karibuni, hasa kizazi cha GenZ, hakijaona thamani ya kuenzi utamaduni na sanaa zetu, hivyo kuwa njia ya kuua Utanzania wetu kwa kasi kubwa.

Vijana hawa – wengi wanatambua historia na tamaduni za nje; hasa Ulaya na Marekani na kutojua chembe ya chimbuko lao. Hali hiyo ni hatari na kuwa matarajio ni kuona Makonda na wasaidizi wake wanakwenda kurekebisha hali hii.

Katika michezo, imani ya Pambazuko ni kubwa zaidi kwani hapo Makonda ndiyo “nyumbani” kwake. Ni kijana bado anayefahamu wenzake wanahitaji nini. Anapenda burudani na hapo tunaamini atafanya vyema zaidi kupaisha hata michezo mingine “iliyolala na kulazwa na sisi wenyewe”.

Pambazuko tunamtakia kila heri Makonda katika majukumu yake mapya – na kumhimiza ajifunze zaidi. Atende haki na kuibua mapya kwa neema ya Tanzania na watu wake, kwani eneo alilokabidhiwa, linabeba majukumu ya kuponya taifa.




*Waziri Mkuu, Dkt. Mwigulu Nchemba akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Chukwani Zanzibar alipotembelea chumba cha kompyuta baada ya kuzindua wakati wa Maadhimisho ya Miaka 62 za Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar hivi karibuni. (Picha na Ofisi ya Waziri Mkuu)*


# Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **"HABARI"** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: info@pambazuko.or.tz** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **"HABARI"** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

Unaweza kusoma gazeti hili kupitia tovuti ya **www.rifaly.com**



**WASILIANA NA CHUMBA CHA HABARI; 0784 211 716**

*Tunapatikana Pambazuko Initiative Office, Mtaa wa Mpakani A – nyuma ya Jengo la Sayansi. Kitalu Namba 435; Plot 44. Mawasiliano ya ofisi: Simu +255 744 768263 na Email: info@pambazuko.or.tz*

# Dunia: Hapa na pale

## Pongezi zamponza Ruto

HATUA ya Rais wa Kenya, William Ruto (pichani) kupongeza ushindi wa Rais wa Uganda, Yoweri Museveni, kumewaingiza vijana barabarani wakimlaani.

Watumiaji wa mitandao ya kijamii, hasa vijana, wameonekana katika baadhi ya mitaa ya Jiji la Nairobi, wakieleza kuwa kiongozi wao, Rais Ruto hakupaswa kumpongeza Museveni kwa kutangazwa mshindi wa urais kwa madai kuwa uchaguzi wa Januari 15, mwaka huu, haukuwa wa haki na huru.

Vijana hao walieleza kushangazwa na pongezi hizo wakisema kulikuwa na kila dalili kwamba uchaguzi mkuu wa Uganda uligubikwa na dhuluma na vitisho dhidi ya mpinzani mkuu wa Museveni (81), Bobi Wine, 43.



"Baada ya kutangazwa rasmi kwamba umechaguliwa tena kwa muhula mwingine, nakupa pongezi kwa niaba ya serikali na niaba ya Wakenya," Rais Ruto aliandika kwenye chapisho lake kwenye mtandao wa X.

## Mtoto wa Museveni kiboko

MKUU wa Majeshi wa Uganda, Muhoozi Kainerugaba, amesema kuwa ushindi wa baba yake, Yoweri Museveni, umeidhihirishia dunia kuwa "Uganda ni yake."

Kwamba ushindi wa zaidi ya asilimia 70, unamuweka Museveni kuwa kiongozi aliyewahi kupendwa zaidi na Waganda na kuwa "hakuna wa kumuondoa madarakani."

Muhoozi ambaye amekuwa gumzo mara kwa mara kutokana na maneno anayoandika kupitia mitandao ya kijamii, amekuwa akitishia"kumchakaza" yeyote anayethubutu kuharibu taswira ya baba yake.

"Ikiwa kuna mtu anataka kuumia, basi ajaribu kuvuruga taswira ya mzee, mimi sitamuacha na atakiona cha mtema kuni na kujuta kuzaliwa," amesema Muhoozi.

## Tume yaomba radhi wapigakura

TUME ya Uchaguzi ya Uganda imelazimika kuomba radhi wapigakura kwa kuchelewa kuanza kwa zoezi hilo lililofanyika Januari 15, 2026

Katika taarifa yake, tume hiyo imeeleza kuwa kulitokea hitilafu kwenye mitambo yake ya kielektroniki, hivyo kushindwa kuanza kuandikisha wapigakura nchi nzima.

Hatua hiyo inaelezwa kuwa ni nadra sana kutokea kwa nchi za Afrika, ambako tume zimekuwa zikionekana kuongozwa na kusimamiwa na vyama tawala, ambavyo – mara zote havitaki kuachia madaraka, hata kama vinakataliwa na wananchi.

Katika taarifa iliyotolewa kupitia mtandao wa kijamii wa X, tume hiyo ilisema ililazimika kuagiza wasimamizi wa uchaguzi kuanza kutumia njia za zamani za kuandikisha kura, ingawa wataalamu walirekebisha hitilafu hiyo na kuendelea na upigaji kura.

## Ukimya wa Putin wahojiwa

UBABE wa Marekani kuingia nchi zingine, umeibua wasiwasi kutoka kwa wanazuoni na wachambuzi wa siasa za dunia wakihoji, mbona mbabe mwingine wa dunia yuko kimya?

Inaelezwa na wachambuzi hao kwamba ukimya wa Russia dhidi ya uvamizi wa Marekani nchini Venezuela na kumkamata kiongozi wa nchi hiyo na mkewe na kuwashitaki Marekani, kunaonyesha kuwa Russia inakubaliana na hatua hiyo ya Marekani.




Zamani ikiwa Marekani ingefanya vitendo vya uchokozi katika ardhi ya kigeni, kungekuwa na jibu la haraka na kali kutoka Russia, lakini, hali inaonekana tofauti kidogo kwa sasa.

Marekani ilifanikisha kumteka Rais wa Venezuela, Nicolas Maduro na mkewe na sasa inaeleza kutaka kuivamia Greenland.

Na Mzee TAI

# Nauona 2026 ukibeba matumaini

NAAMINI kabisa kwamba ndugu zangu na Watanzania wenzangu, tumeupokea mwaka mpya, 2026 kwa bashasha na matumaini mengi yenye afya.

Hata kama kila mwaka mpya – hasa siku ya kwanza kila mmoja hubeba matumaini ya kuwa mpya, hata kama mazingira, mara nyingi huleta historia tofauti, lakini tusihofu.

Mwaka huu ni kama sherehe yenye rangi nyingi za kuvutia, ambapo kila mmoja wetu anatamani kupata furaha, mafanikio tele, na baraka zisizo na kikomo.

Hebu twende pamoja tukakumbushane kuwa mwaka huu siyo wa kuruhusu mabishano yasiyo na msingi, bali ni mwaka wa kuleta pamoja jamii zetu na kuponya majeraha ya kisiasa na uchaguzi.

Katika mwaka huu, hebu tufanye vizuri tunavyoweza! Ni wakati wa kutafakari na kujikumbusha kuhusu umuhimu wa amani.

Nani anahitaji kuingia katika vita vya maneno, wakati tunaweza kuwa na vikao vya mashauriano tukiwa taifa moja la Watanzania!

Naomba tuamke na kufikiria kuwa amani na haki ni kama kisima cha maji cha Kijiji; wote tunakitegemea kuishi.

Ni vyema mwaka huu tukaingia ndani ya vikao vya mazungumzo ili kuijenga na kuiimarisha Tanzania yetu.

Na siyo tu kuhusu amani na haki; huu ni wakati wa kusameheana! Tukumbuke, msamaha siyo tu maneno matamu, bali ni kuchukua hatua. Tuweke tofauti zetu kando.

Mimi Mzee Tai nauona mwaka huu kuwa wenye heri, baada ya kutokea madhila ya uchaguzi mkuu ambapo watu walipotezewa maisha yao, kujeruhiwa na mali kuharibiwa.

Hebu tuone mwaka huu kuwa mwaka wa kutengeneza majeraha – siyo tu ya kisiasa, bali hata ya moyo. Tusikubali majeraha yadharauliwe kama vile ni mashaka ya ng'ombe wa jirani!

Kila mmoja wetu anahitaji kutenda majukumu yake kwa weledi, huku tukiwa na furaha na kuhamasisha wengine. Acha tuwe mfano wa uzuri katika jamii zetu. Tujitahidi kuwa kama nyota zinazong'ara, zikiwa na mwangaza hadi kwenye kona za mbali – siyo tu kwa maendeleo binafsi, lakini pia katika kuimarisha familia zetu na nchi yetu.

Hebu fikiri, unavyofanya kazi kwa bidii na kujituma, unasaidia siyo tu mkeo au mumeo, bali pia umejitolea kwa taifa zima kama mfalme au malkia!

Kila mmoja wetu akumbuke kuwa anaweza kubeba mzigo, lakini ni wachache wanaweza kubeba furaha kwa pamoja. Pia, tunapofanya jambo lolote, tufanye kwa moyo mmoja, tukitabasamu.

Mwaka mpya ni fursa ya kujiweka sawa, kujiandaa vizuri na kusherehekea! Tuanze mwaka huu kwa matumaini, upendo na umoja, tukiwa na dhamira ya kuwa Watanzania bora – bila kujali tofauti zetu.

Karibu mwaka 2026! Tuwe pamoja katika amani, upendo, na maendeleo – tukiwa na tabasamu kama ishara ya mshikamano wetu.



Habari Kuu

# Mabilioni kutumika 'kusafisha nyota' ya Tanzania



Na Mwandishi WETU

SERIKALI ya Tanzania imeingia mkataba na kampuni moja ya Marekani kwa lengo kubwa moja; kusafisha taswira ya nchi baada ya kutokea kwa machafuko ya Oktoba 29, mwaka jana – 2025.

Kiasi cha shilingi bilioni 2.72 zitatumika kulipa Kampuni ya Ervin Graves Strategy Group LLC, ambayo hutoa huduma ya ushawishi na kujenga taswira chanya.

Gazeti la Pambazuko ambalo limeona mkataba huo, unaeleza kwamba moja ya majukumu makubwa ya kandarasi hiyo ni kuboresha taswira ya Tanzania baada ya mgogoro wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 na kuvutia uwekezaji wa kimkakati hususan kwenye sekta ya madini.

Duru za kisiasa ndani na nje ya Tanzania zinabainisha kuwa hatua na uwekezaji huu unalenga kusaidia kurekebisha taswira ya Tanzania kimataifa na hasa kuisafisha Serikali ya Awamu ya Sita ya Tanzania machoni mwa utawala wa Rais wa Marekani, Donald Trump.

Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ndiyo iliyosaini mkataba huo wa miaka miwili na kampuni ya Ervin Graves Strategy Group LLC. Kampuni hiyo ina ukaribu zaidi na chama kinachotawala Marekani kwa sasa, Republican.

Mkataba huo ulioanza kutekelezwa rasmi Desemba 15, 2025, umesainiwa na Katibu Mkuu - Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Dkt. Samwel Shelukindo na Rais na Mtendaji Mkuu wa Ervin Graves Strategy Group LLC, Tom Graves.

Mkataba huo wenye thamani ya dola za Marekani milioni 1.08 (takribani shilinigi 2.72) - umesajiliwa chini ya Sheria ya Marekani ya Uwakilishaji wa Maslahi ya Kigeni (FARA).

Kwa mujibu wa mkataba huo, Kampuni ya Ervin Graves italipwa dola 45,000 kwa mwezi (takribani shilingi milioni 113.5).

Inaelezwa kuwa mkataba huo utajikiza zaidi kwenye ushawishi wa wawekezaji wa sekta za kimkakati ikiwamo madini.

Kwa sasa, duru hizo zinaonekana kutoridhishwa na mwenendo wa masuala ya demokrasia, uhuru wa kisiasa, utawala bora na haki za msingi nchini.

Jarida la Africa Intelligence (toleo la Januari 16, 2026) linaeleza kuwa uamuzi wa kuajiri Ervin Graves unalenga kupunguza mvutano wa kisiasa na kurejesha uhusiano mwema na duru za karibu za Rais Trump, wakati Tanzania ikiendelea kukabiliwa na shinikizo la kimataifa kufuatia dosari za uchaguzi wa 2025.

Kwa mujibu wa jarida la Africa Intelligence, Ervin Graves itaisafisha Serikali ya Tanzania na kusaidia kuiboresha taswira ya Tanzania kwa kutekeleza mkakati unaojulikana kama Third-Party Validation Strategy, ambapo badala ya serikali kujitetea moja kwa moja, watu na taasisi huru zenye ushawishi - wakiwemo wasomi, watafiti na taasisi za sera, ndio watakaotumika kuzungumzia Tanzania kwa mtazamo chanya.

Ndani ya mkataba huo, kampuni hiyo ya Marekani inalenga kuwashirikisha wanasiasa, taasisi za tafiti, na wasomi kuizungumzia Tanzania kwa njia chanya.

Pia, kampuni hiyo itakuwa na kazi ya kuratibu mikutano, mazungumzo na matukio ili maoni ya Tanzania yaonekane kutoka kwa watu au taasisi zenye kuaminika zaidi ndani na nje ya Marekani.

Inaendelea Uk.7

# Mabilioni kutumika 'kusafisha nyota'...

Inatoka Uk. 6

Lengo la kuvutia wawekezaji wa Marekani

Mbali na kusafisha jina na kuboresha taswira ya Tanzania kimataifa, sehemu kubwa ya mkataba huu imejikita katika masuala ya kiuchumi.

Inaelezwa kuwa Tanzania imeamua kuchukua mkondo wa kidiplomasia kwa kutumia ushawishi wa kulipwa, siyo tu kudhibiti athari za kimataifa - hasa Marekani ambako mitazamo ya sera kuhusu serikali bado inaathiriwa na masuala ya Uchaguzi Mkuu wa 2025 - bali pia kushawishi na kuvutia uwekezaji wa kimkakati katika sekta ya madini.

Mkazo umewekwa hususan kwenye madini adimu na muhimu (strategic minerals) yanayohitajika kwa kiwango kikubwa nchini Marekani.

Hatua hii ya Tanzania pia inatazamwa kama fursa ya kimkakati kwa Marekani katika ushindani wake unaoongezeka na China barani Afrika, hasa katika jitihada za kuhakikisha upatikanaji wa rasilimali muhimu kwa viwanda, teknolojia za kisasa na usalama wa kiuchumi.

**Uchaguzi wa 2025: Mzizi wa tatizo**

Hatua hii ya kidiplomasia inajiri katika mazingira nyeti ya kisiasa, kufuatia Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2025 uliogubikwa na masuala kadhaa ikiwamo kutoshiriki kwa chama kikuu cha upinzani, Chadema, kuwekwa kizuizini kwa kiongozi wake, Tundu Lissu na hata maandamano ya vijana wa Gen Z yaliyosababisha vifo, majeruhi na uharibifu wa mali.

"Katika mazingira haya magumu ya kisiasa na kidiplomasia, serikali ilijikuta ikiwa na chaguo finyu, na ikaamua kuchukua mkondo wa diplomasia usio wa kawaida kwa kutumia ushawishi wa kifedha kama nyenzo ya kudhibiti na kupunguza mtazamo hasi wa jumuia ya kimataifa kuhusu matukio ya ndani ya nchi…"

"Hatua hii imelenga kulinda taswira ya Serikali ya Awamu ya Sita, na kwa upana zaidi, heshima na maslahi ya Tanzania katika medani ya kimataifa," amesema kiongozi mmoja wa moja ya jumuia kubwa za wafanyabiashara nchini.




*Wakazi wa maeneo ya Mbezi kwa Msuguri wakiangalia ajali ya Lori lililoacha njia na kuingia upande wa pili wa barabara ya Morogoro na kusababisha majeruhi wa wawili waliokuwa wakisubiri kuvuka, Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. (Na Mpigapicha Wetu)*

Habari

# Trilioni 10 zawekeza maboresho bandari




*Waziri wa Uchukuzi Prof. Makame Mnyaa Mbarawa akihojiwa na waandishi wa habari wakati wa ziara yake. (Picha na Mpigapicha Wetu).*

**Na Mwandishi WETU**

SERIKALI imewekeza zaidi ya shilingi trilioni 10.08 kwa ajili ya kuimarisha na kuboresha bandari za Tanzania.

Waziri wa Uchukuzi, Profesa Makame Mnyaa Mbarawa, amesema Rais Samia Suluhu Hassan ameidhinisha kiasi kicho cha fedha kwa kutambua umuhimu, ulazima na uhalali wa Tanzania kuwa na bandari bora kwa ajili ya kuchochea maendeleo.

Kiasi hicho cha fedha kimewekezwa katika miradi 22 ya ujenzi, ikiwa ni kwa ajili ya upanuzi na maboresho ya bandari kote nchini. Hii ni sehemu ya mkakati wa kuimarisha miundombinu ya usafiri wa majini na kukuza uchumi wa taifa.

Profesa Mbarawa amesema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa ziara yake ya kikazi ya kutembelea na kukagua maendeleo ya ujenzi wa Bandari mpya ya Mbamba Bay, iliyopo Wilaya ya Nyasa, Mkoa wa Ruvuma.

Akizungumza na viongozi wa serikali, wataalamu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) na wananchi wa eneo hilo, Profesa Mbarawa amesema uwekezaji huo mkubwa unaonyesha dhamira ya dhati ya Rais Samia ya kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha biashara na usafirishaji katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kusini.

Ameeleza kuwa ujenzi wa bandari mpya ya Mbamba Bay kwa shilingi bilioni 81 ni miongoni mwa miradi ya kimkakati inayotekelezwa chini ya Wizara ya Uchukuzi, hususani katika Maziwa Makuu, kwa lengo la kuimarisha biashara ya kikanda na usafiri wa majini katika Ziwa Nyasa.

Naibu Mkurugenzi Mkuu wa TPA Mhandisi Dkt. Baraka Mdima, akizungumza kwa niaba ya mkurugenzi wake mkuu amesema mradi wa Bandari ya Mbamba Bay umefikia asilimia 47 ya utekelezaji wake, na unaendelea kutekelezwa kwa kuzingatia viwango vya kitaalamu, usalama na utunzaji wa mazingira.

Dkt. Mdima aliongeza kuwa kukamilika kwa bandari hiyo kutachochea biashara kati ya Tanzania na nchi jirani za Malawi na Msumbiji, sambamba na kuongeza ajira, uwekezaji na fursa za kiuchumi kwa wananchi wa Wilaya ya Nyasa na Mkoa wa Ruvuma kwa ujumla.

Mhandisi Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Mbamba Bay kutoka TPA, John Paul, alitoa maelezo ya kitaalamu kuhusu maendeleo ya mradi, akibainisha kuwa kazi zinaendelea vizuri na kwa mujibu wa ratiba iliyopangwa.

Katika ziara hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Brigedia Jenerali Ahmed Abbas, alipongeza serikali kwa kuendelea kupeleka miradi mikubwa ya maendeleo mkoani humo, akisema bandari hiyo itakuwa chachu ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa wakazi wa Nyasa na maeneo ya jirani.

Mradi wa ujenzi wa bandari mpya ya Mbamba Bay unatarajiwa kuimarisha usafiri wa majini katika Ziwa Nyasa, kuchochea biashara kati ya Tanzania na Nchi jirani zikiwemo za Malawi na Msumbiji na kuimarisha nafasi ya Tanzania katika biashara ya kikanda.

# Kiini macho Sheria ya Manunuzi

**Na Elizabeth HOMBO**

PAMOJA na Sheria ya Manunuzi ya Umma kuelekeza kuwa asilimia 30 ya thamani ya bajeti ya manunuzi yote ya umma zitengewe kwa ajili ya makundi maalum, hilo halitekelezwi na kuifanya sheria hiyo kuwa 'kiini macho.'

Ufuatiliaji uliofanywa na Pambazuko umebaini kuwa ni kiasi kidogo zaidi cha manunuzi kinatengwa kwa ajili ya makundi maalum yanayohusisha wanawake, vijana, wazee na watu wenye ulemavu.

Sheria hiyo ilitungwa na kuweka upendeleo huo maalum baada ya kubainika kuwa makundi hayo hayanufaiki na manunuzi yanayofanywa na serikali.

Kila mwaka serikali hutumia zaidi ya asilimia 30 ya matumizi yake kufanya manunuzi ya bidhaa, vifaa, kazi na huduma.

Serikali yenyewe inakiri kupitia ripoti mbalimbali ambazo Pambazuko imezichambua kuwa ni asilimia mbili tu ya thamani ya manunuzi yote nchini ndio hutengwa kwa ajili ya makundi hayo.

Tathmini ya mifumo ya manunuzi ya umma pamoja na ripoti ya Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), inabainisha kuwa ni asilimia mbili tu ya taasisi zilizokaguliwa ambazo zilitimiza takwa la kisheria la kutenga asilimia 30 ya manunuzi kwa makundi maalum.

Pia ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2020/21, inaonyesha kuwa taasisi zilizokaguliwa hazikutenga kiasi chochote cha manunuzi kwa makundi maalum.

**Sheria inasemaje**

Kifungu cha 64(1) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2023, kinazitaka taasisi zote za umma kutekeleza mifumo ya manunuzi yenye ujumuishaji kwa kuweka utaratibu maalum wa kutenga sehemu ya zabuni za umma kwa makundi maalum.

Makundi hayo maalum ni pamoja na wanawake, vijana, wazee na watu wenye ulemavu, lengo likiwa ni kukuza usawa wa kijamii na uwezeshaji wa wananchi kiuchumi.

Aidha, kifungu cha 64(2) cha sheria hiyo kinazipa mamlaka za udhibiti wa manunuzi, ikiwemo PPRA, kutoa kanuni na miongozo ya kuhakikisha utekelezaji wa sharti hilo unafanyika kwa ufanisi na uwazi.

Kwa kuzingatia matakwa hayo ya kisheria, PPRA imeweka miongozo inayotaka kila taasisi ya umma kutenga angalau asilimia 30 ya thamani ya manunuzi ya umma kwa ajili ya makundi maalum.

Matakwa hayo ya kisheria ni sehemu ya mkakati wa kitaifa wa kutumia manunuzi ya umma kama chombo cha kupunguza umasikini, kuongeza ajira na kukuza biashara za wananchi wa ndani.

Kifungu cha 35(1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2024, kinalazimisha taasisi za ununuzi kutoa upendeleo wa kipekee wa asilimia 30 ya manunuzi yake ya kila mwaka ya bidhaa, kazi na huduma kwa makundi maalum yaliyopo katika eneo lake.

Kanuni ya 33(1), inaeleza vigezo vya sifa kwa kikundi maalum kufaidika na mpango huo, ikiwemo kuwa na usajili unaotambulika, asilimia 70 ya wanachama wake kuwa wa kundi husika na kuwa na uwezo wa kutekeleza mkataba.

Nayo Kanuni ya 34(1) inataka makundi maalum kusajiliwa na vyombo husika vinavyohusika na uwezeshaji wa makundi hayo kabla ya majina yao kuwasilishwa PPRA kwa ajili ya kuingizwa kwenye kanzi data ya upendeleo.

Inaendelea Uk. 14

Tafakuri ya Bagonza



Na Dkt. Benson BAGONZA

# Kihongosi ana hoja, lakini kaishika juu-chini



Kenan Kihongosi

NIMEMSIKILIZA Katibu Mwenezi na Itikadi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Kenani Kihongosi akimzungumzia Mzee Warioba.

Napenda kwanza, nitangaze mgogoro wa maslahi. Nampenda huyu kijana. Huwa ni mnyenyekevu na msikivu. Haaniki madhaifu yake kama sisi wengine. Akisema jambo napenda kumsikiliza.

Anasema Mzee Warioba astaafu vizuri. Pia kwamba Mzee Warioba ana chuki na viongozi. Nimetafakari haya kuhusu maneno yafuatayo ya Kihongosi.

Kwamba Mzee Warioba aliishastaafu. Siyo sehemu ya serikali hata kama ni mwanachama wa CCM. Mzee huyu ndiye mstaafu halisi na pekee. Wengine mnaodhani wamestaafu, bado hawajastaafu ndio maana wako kimya maana wanafungwa na kanuni ya uwajibikaji wa pamoja.

Kwamba Mzee Warioba hana chuki na viongozi. Anawapenda kama Baba wa Taifa alivyowapenda kina Ali Hassan Mwinyi, Horace Kolimba, John Malecela na Edward Lowassa. Kama raia na mstaafu wa kweli, aliwaambia ukweli kwa upendo kuliko kujificha na kunung'unika pembeni. Mzee Warioba ana upendo mkubwa kwa viongozi walio zamu.

Badala yake, Mzee Warioba anaweza kuwa anachukiwa ama na viongozi au na CCM. Kwa kuwa msemaji wa chama kasema, ni sahihi kuamini kuwa ipo chuki mahali fulani. Imani ya 8 ya TANU na CCM inasema, "Nitasema kweli daima, fitina kwangu mwiko". Mzee Warioba bila hofu wala aibu amesimamia ukweli, haki na uwazi. Kama kwa kufanya haya anastahili kulipwa maonyo haya, namshauri ayapokee bila kinyongo.

Kwamba vyama vyote vya siasa hapa nchini, ni vyama vya viongozi kuliko kuwa vyama vya wanachama. Mzee Warioba ni muumini aliyepitwa na wakati kwa kuamini vyama ni mali ya wanachama.

Hata hivyo, kuna siku vyama vyote vitawajitaji akina Mzee Warioba wengi ili dhambi za viongozi zibakie kuwa zao na zile za serikali zisiwe dhambi za vyama. Vyama viongoze, visiongozwe. Tafakari.

Kwamba baadhi ya mawaziri wakuu waliomfuata Warioba, walichoshwa na dharau na uonevu mbalimbali na kuamua kuhamia vyama vya upinzani.

Mwingine aligombea urais akatukanwa matusi yote mpaka kuitwa Mwarabu wa chama cha Hizbu. Mwingine aliwasifia Chadema kuwa wanajua kujenga hoja, akaitwa na kuonywa kiutu uzima. Ni maisha magumu mtu mzima kuishi umefarakana na dhamiri yako. Mzee Warioba ameamua kuwa mtumwa wa dhamiri. Aheshimiwe.

Nampongeza rafiki yangu Kenani, lakini nahisi hoja hii ameishika kichwa chini na miguu juu.

Akipenda amtembelee Mzee Warioba. Ajifunze na amfundishe imani mpya za CCM. Enzi zetu, tulipenda kumtembelea na kujifunza kujenga hoja. Angefufuka hayati Mohamed Seif Khatibu angekueleza.

Ila ninakupongeza, unajitahidi kujenga hoja kuliko Wajaluo wote kwa umoja wao.

***Mwandishi wa safu hii ni Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Karagwe. Ni mchangiaji maalum wa safu na makala ndani ya Pambazuko.***

Na Dkt. Hellen Kijo BISIMBA



Kona ya Dkt. Bisimba

# Mwaka 2026 bado tumejichimbia mchangani?

NAPENDA niwatakie wote heri ya mwaka 2026. Mwaka 2025 hatimaye umepita ila sioni kuwa ni ndwele kwani yaliyotusibu yako mioyoni bado.

Nilimkumbuka Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, hasa baada ya mambo yaliyotusibu Oktoba 29, 2025 na siku na miezi iliyofuata.

Ninamkumbuka Mwalimu kwa kuwa katika kipindi cha utawala wake yako mambo magumu yaliyotokea ikiwemo wanafunzi wa chuo kukataa kwenda kujiunga na JKT na kuamua kuandamana huku wakitamka maneno magumu.

Lakini, majibu yake hayakuwa kifo, kulikuwa na sauti na sheria. Ningetamani kusikia sauti ya Mwalimu pale watu walipotamka kwa kishindo ‘bila mabadiliko hakuna uchaguzi,’ au pale walipoongea kupinga utekaji na mauaji ya raia, na pale walipojaribu kukosoa mwelekeo wa chama na serikali.

Sijui ambacho Mwalimu angesema, lakini natambua jinsi ambavyo angezungumzia hayo hata walioinua hizo hoja wangempigia kofi.

Najua wapo wanaonishangaa, lakini tujiulize tumeuanza mwaka wa 2026 tunaelekea wapi?

Nimeona Marekani ikichukua hatua kuingia nchi nyingine huru na kumteka rais na mke wake na bado wanashikiliwa ndani ya nchi hiyo.

Wapo wanaoona hili ni suala baya sana la uvunjifu wa haki na uhuru wa taifa jingine. Na hii ni kweli, ila nimewaona watu waliofananisha na baadhi ya matukio ya hapa kwetu kwenye mrengo wa uvunjifu wa haki na sheria kuwa wapo wanaovunjiwa haki kwa aina hiyohiyo.

Jambo jingine ni furaha iliyopatikana timu yetu ya soka; Taifa Stars ilipovuka kuingia kwenye 16 bora kwenye fainali za Afcon, ila wapo waliosikitika kwa kuwa hawakufurahishwa na walitamani timu yetu ishindwe, hii inatia shaka kama tuko pamoja.

Lakini timu yetu hiyo ilipocheza na timu ya Morocco Januari 4, na kufungwa bao 1-0, watu wengi walilalamika jinsi refa alivyoipendelea timu ya Morocco.

Hapo nikaona hadi katuni zikifananisha hiyo hali na refa wa uchaguzi mkuu wa Tanzania kuwa naye hakutenda haki wamefikia hata kusema mradi palikuwa na amani uwanjani masuala ya haki tuachane nayo wakikejeli maneno yanayozungumzwa hapa nchini kuhusu amani na haki.

Hapo pia bado hatupo pamoja.

Jingine ni hili la watu waliosemekana waumini wa Kanisa Katoliki walioongozana kwenda kwa Balozi wa Papa kumshtaki Askofu Ruwaichi na Padre Charles Kitima wa Kanisa Katoliki. Hawa inaonekana wanapelekwa kwa Papa kwa kuwa wasema kweli wa masuala yanayoendelea nchini.

Lakini kilichoshangaza ni kuwa watu hao waliandamana hadi ofisini kwa balozi huyo bila kuzuiwa.

Askofu Benson Bagonza amewapongeza polisi kwa hilo na kuwataka wakitokea wengine wanaandamana wasiwazuie.

Lakini, miongoni mwa waandamanaji hao wapo waliobainika kuwa siyo wakatoliki. Mavazi yao na nyimbo walizoimba haziendani kabisa na tamaduni za Kikatoliki.

Sasa wakati bado tuko siku chache za mwanzo wa mwaka, tujiulize, je mwaka huu utuletee nini?

Mwelekeo wa kuganga ya 2025 mbona hauonekani? Bado tumejichimbia mchangani? Tunaonekana!

Naitamani Sauti ya Mwalimu.

***Mwandishi wa safu hii ya kila wiki, ni mwanaharakati wa demokrasia, haki za binadamu na mwanazuoni wa falsafa ya sheria. Anapatikana kwa namba 0713 337240.***

# Mfanyabiashara avuruga Jiji D’Salaam



Na Mwandishi WETU

MFANYABIASHARA Gervaz Shayo anadaiwa kuvamia eneo la wazi la ukanda wa kijani (green belt) lililotengwa kisheria katika Mtaa wa Kibaga, Kata ya Kinyerezi, Wilaya ya Ilala, Dar es Salaam.

Mfanyabiashara huyo anaendelea na ujenzi katika eneo hilo licha ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, kupitia Idara ya Mipango Miji, kutoa notisi inayobainisha kuwa ujenzi unaoendelea katika eneo hilo hauna kibali, hivyo ni batili.

Mmoja wa maofisa waandamizi katika Idara ya Mipango Miji Kanda ya Kinyerezi katika Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, ambaye hakupenda kuandikwa jina lake gazetini, ameliambia Pambazuko kuwa, hakuna kibali kilichotolewa kwa mtu yeyote kufanya ujenzi kwenye eneo hilo.

Akasema hivi sasa halmshauri yake inajiandaa kuchukua hatua kwa mtu yeyote anayekiuka sheria na utaratibu kupitia ujenzi huo.

Wakati hali ikiwa hivyo, wananchi wanaoishi jirani na eneo hilo wamemtupia lawama Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, kwa kushindwa kuchukua hatua kulinda maeneo yasivamiwe, jambo ambalo linatishia uharibifu mkubwa wa mali na hata kugharimu uhai wa watu endapo yatatoka mafuriko.

Kwa mujibu wa Sheria za Mipango Miji, eneo hilo na mengine kama hayo, yametengwa kisheria na hayaruhusiwi kutumika kwa ajili ya makazi na shughuli zingine isipokuwa bustani ili yaendelee kuwa na mwonekano wa kijani.

Aidha, Pambazuko limeona nakala ya notisi ya zuio la ujenzi wa eneo hilo, ikiwa na utambulisho wa; Kumb No DCC/HD.101/31 iliyotolewa Novemba 19, 2025 kutoka kwa Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam kwenda kwa Gervas Shayo, ikimpa amri ya kubomoa na kuondosha ujenzi uliofanyika kinyume cha sheria katika eneo hilo.

Notisi hiyo ilisainiwa na Mhandisi Lusekelo A. Mwakyami kwa niaba ya mkurugenzi, inasema; “Kwa kuwa umejenga ukanda wa kijani ambalo ni kosa chini ya kanuni ya 139 (1) ya serikali za mitaa, mamlaka za miji, (udhibiti wa ujenzi) ya mwaka 2008, unaamriwa ndani ya siku 14 tangu kupokea amri hii uwe umebomoa na kuondosha ujenzi huo.

Notisi hiyo inaonyesha ilimfikia Shayo Novemba 24, 2025 na kuisaini huku jina la shahidi likisomeka, Devotha T. Mobhitete.

“Kinyume cha hivyo Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam itatumia mamlaka yake chini ya kanuni 139 ya sheria tajwa kutekeleza amri hiyo na hatimaye kukudai gharama za uvunjaji, uondoshaji, au marekebisho yoyote yaliyofanywa kwa mujibu wa kanuni, na iwapo utakaidi, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam itakushtaki mahakamani”, inasema sehemu ya notisi hiyo.

**Kanuni inavyosema**

Kanuni ya 139(1) inaweka wajibu kwa mtu yeyote anayejenga, kurekebisha au kubadilisha jengo ndani ya mamlaka ya mji/manispaa kupata kibali cha ujenzi kutoka kwa mamlaka husika kabla ya kuanza kazi.

Kwa vitendo, kanuni hii inakataza ujenzi bila kibali kutoka kwa mamlaka husika, inalazimisha uwasilishaji wa michoro na nyaraka (ramani za usanifu, miundombinu, na uthibitisho wa umiliki/ruhusa ya ardhi) kwa ajili ya mapitio na idhini.

Inaendelea Uk. 13

# Mfanyabiashara avuruga...

Inatoka Uk. 12

Aidha, kanuni inampa mamlaka mkurugenzi au ofisa ujenzi wa mji kusimamia, kukagua na kuchukua hatua endapo ujenzi unakiuka masharti na inalenga usalama, mipango miji na maslahi ya umma, ikijumuisha ulinganifu wa matumizi ya ardhi, viwango vya kiusalama na mazingira.

Madhara ya kukiuka kanuni hii ni pamoja na kusimamishwa kwa ujenzi, adhabu/faini, au kubomolewa kwa jengo kulingana na taratibu za halmashauri na sheria husika.

Lakini ikiwa imepita miezi miwili tangu kutolewa notisi hiyo, baadhi ya wananchi wa Mtaa wa Kibaga wameeleza kushtushwa kwani ujenzi wa nyumba unaendelea kwenye eneo hilo, huku mamlaka husika zikishindwa kuchukua hatua kuzuia uvunjwaji huo wa sheria.

Mmoja wa wakazi wa eneo hilo, Ibrahim Nyakyoma, anasema wanashangazwa na ukimya wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam licha ya kupelekewa taarifa tangu ujenzi huo unaanza, lakini haukuchukua hatua zozote kuzuia uharibifu huo wa mazingira.

"Hii inaonyesha Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ameshindwa kulinda maeneo haya na kuruhusu uvamizi wa holela…"

"Mvamizi ameanza kujenga msingi, nyumba hadi ukuta na anajenga usiku na mchana hadharani, si kwa kificho, lakini hachukuliwi hatua, hii maana yake ni nini?

"Makazi yetu haya yamepimwa si makazi holela, yana ramani zake, hivyo yeyote akitaka kufanya ujenzi lazima awe na vibali kutoka halmashauri husika," anasema

Mkazi mwingine anahoji; "eneo hilo lilikwishalipiwa fidia na serikali kwa wamiliki wa asili kupitia mradi wa Songas, je, huyu anayejenga kapata wapi kibali, au kuna jambo linafichwa?"

Pambazuko lilifika katika eneo hilo na kushuhudia ujenzi wa nyumba ukiendelea karibu na mfereji mkubwa wa maji unaotenganishwa na barabara ya lami ya Kinyerezi na Gongolamboto.

Pia lilimtafuta Shayo ili kupata maoni yake, ambapo alisema amekabidhi majukumu yote kwa mwanasheria wake aliyemtaja kwa jina la Thomas Yohana.

Pambazuko lilimtafuta na kumpata wakili huyo na alipoulizwa iwapo mteja wake anavyo vibali, Yohana alijibu kwa swali kwa mwandishi endapo amepata majibu ya suala hilo kutoka halmashauri ya jiji kwa maandishi.

**Yohana:** Ulipokwenda halmashauri walikupa majibu gani?

**Mwandishi:** Walisema mteja wako hana kibali.

**Yohana:** Hayo majibu wamekupa kwa maandishi? Kama hawakukupa kwa maandishi, basi siwezi kukujibu kitu chochote. Akakata simu.

Kwa upande wake, Mtendaji wa Serikali ya Mtaa wa Kibaga, Athuman Yassin, alikiri kuwapo ujenzi unaoendelea katika eneo hilo la ukanda wa kijani, lakini alisema hawezi kuchukua hatua zozote mpaka apate maelekezo kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashuri ya Jiji la Dar es Salaam.

"Ni kweli suala hilo lipo, lakini siwezi kuchukua hatua zozote. Nasubiri idhini ya Mkurugenzi kwa kuwa kuna timu ilikuja kuchunguza suala hilo, nadhani tuingoje imalize kazi yake," alisema mtendaji huyo wa mtaa.

Wakati hali ikiwa hivyo, Pambazuko limeona nakala ya kibali kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ilala ya Julai 31, 2013 kwenda Kampuni ya Group Five Earthworks (T) LTD cha kupanda maua, miti na kuzungushia uzio eneo hilo la ukanda wa kijani Kinyerezi.

Pamoja na mambo mengine, kibali hicho kilitolewa baada ya kufanyika ukaguzi kwenye eneo husika ulioshirikisha maofisa mazingira na mipango miji wa Manispaa ya Ilala ambao ulibaini kuwapo uvunjwaji mkubwa wa sheria ya mazingira namba 20 ya mwaka 2004.

"Ukaguzi huo pia ulibaini kuwapo uvamizi wa ujenzi wa nyumba na uzio kwenye kingo za mifereji ya maji kwenye eneo hilo badala ya kulinda ardhi oevu," inasema sehemu ya kibali hicho kilichosainiwa na Abdon Mapunda kwa niaba ya mkurugenzi wa halmashauri ya Manispaa ya Ilala wakati huo.

Habari

# Kiini macho Sheria ya Manunuzi

> Maofisa manunuzi wengi katika taasisi wameripotiwa kukosa ujuzi na uelewa wa kutosha kuhusu mahitaji ya Sheria ya Manunuzi ya Umma (PPA) kuhusiana na makundi maalum," iliainisha ripoti hiyo.

Inatoka Uk. 9

Vilevile, PPRA imetoa Miongozo ya Ushiriki wa Makundi Maalum, kama ile ya mwaka 2020 na toleo lililofanyiwa marekebisho Oktoba 2023, ili kutoa maelekezo ya kiufundi ya namna ya kutekeleza vifungu hivyo.

**Kiwango kidogo cha utekelezaji**

Hata hivyo, licha ya sheria kutoa upendeleo huo, tathmini ya Mifumo ya Manunuzi (MAPS 2025), imebainisha kuwa ni asilimia mbili tu ya taasisi nunuzi (PEs) zilizokaguliwa ndizo zilizotimiza takwa la kisheria la kutenga asilimia 30 ya bajeti ya manunuzi kwa makundi maalum.

Kwa mujibu wa Ripoti ya CAG ya mwaka 2020/21, kati ya taasisi 86 zilizokaguliwa ni taasisi mbili pekee ndizo zilizotimiza takwa la asilimia 30 kikamilifu huku taasisi tatu zikitenga chini ya asilimia hizo.

Aidha, taasisi 81 sawa na asilimia 94, hazikutenga kabisa kiasi chochote cha bajeti yao kwa ajili ya makundi maalum.

Vilevile jumla ya mamlaka tatu, sawa na asilimia nne, zilikuwa zimetenga kiasi kwa ajili ya makundi hayo lakini kilikuwa chini ya asilimia 30.

**Changamoto**

Pamoja na sheria na kanuni hizo, ripoti ya mifumo ya manunuzi ya umma, zimeainisha sababu kadhaa za kimfumo na kiufundi zinazokwamisha utekelezaji ikiwemo ukosefu wa uelewa wa kisheria.

"Maofisa manunuzi wengi katika taasisi wameripotiwa kukosa ujuzi na uelewa wa kutosha kuhusu mahitaji ya Sheria ya Manunuzi ya Umma (PPA) kuhusiana na makundi maalum," iliainisha ripoti hiyo.

Sababu nyingine ni ukosefu wa sera na mikakati ya kitaifa kwa kuwa hakuna sera madhubuti ya manunuzi na mkakati wa kitaifa unaotoa mwongozo wa kiufundi kwa watekelezaji.

Pia changamoto za kidijitali na mfumo wa NeST kwa makundi maalum kukabiliwa na kutojua matumizi ya teknolojia na vikwazo vya kiufundi katika kutumia mfumo huo.

Vilevile, ukosefu wa mitaji na ujuzi imetajwa kuwa ni sababu nyingine inayokwamisha wajasiriamali wa makundi maalum kwani wana ujuzi mdogo wa kiufundi katika kuandaa zabuni, usimamizi wa manunuzi na kukosa dhamana na mitaji ya kutosha kutekeleza miradi.

Ripoti hiyo imeainisha sababu nyingine kuwa ni ugumu wa taratibu za zabuni kwa michakato ya manunuzi. Taarifa zinabainisha kuwa taratibu zimeonekana kuwa ngumu na zisizo na uwazi, jambo linalowakatisha tamaa wajasiriamali wa makundi hayo maalum.

**Rushwa nayo yatajwa**

Taasisi ya Utafiti wa Kiuchumi na Kijamii (ESRF) katika utafiti wake wa mwaka 2022 uliohusisha biashara 3,832 zinazomilikiwa na wanawake, ilibaini kuwa ni wanawake 242 tu walioomba zabuni za umma.

Utafiti huo ulibainisha kuwa asilimia 95.9 ya wajasiriamali hao wanawake waliripoti kuombwa rushwa ya fedha na asilimia 8.1 waliombwa rushwa ya ngono pale wanapojaribu kuomba zabuni za umma.

**Athari kubwa**

Kutokutekelezwa kwa asilimia 30 kunazuia makundi maalum kufaidika na fursa za kiuchumi, jambo linalozorotesha juhudi za kupunguza umasikini na kukuza ustawi wa jamii.

Inaendelea Uk. 15

# Kiini macho Sheria...

Inatoka Uk. 14

Athari nyingine ni upotevu wa dhamana ya umma kwa kutokuwepo kwa utekelezaji ambayo huleta picha ya mfumo uliopendelea wazabuni wakubwa tu, hivyo kupunguza uaminifu wa umma katika mifumo ya serikali.

**Idadi ya manunuzi**

Kwa mujibu wa makadirio katika mfumo wa NeST, hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya zabuni zilizopangwa kwenye mfumo wa NeST zilifikia 77,595 zikiwa na thamani ya jumla ya shilingi milioni 30.12.

Idadi ya Mamlaka Nunuzi (PEs) zilizokuwa zimesajiliwa katika mfumo huo wa NeST hadi Juni 2024 ni 1,147, ambazo zote kisheria zinatakiwa kuandaa na kuchapisha Mpango wa Mwaka wa Manunuzi (APP) kupitia mfumo huo.

Kwa kuwa mfumo wa NeST ulianza kutumika rasmi Julai 2023, ripoti za kitakwimu za mwaka mzima kwa kila taasisi zilikuwa bado hazijatolewa kikamilifu wakati wa tathmini hiyo.

**Nini kinafichwa?**

Kuna dalili kuwa kuna mambo yanafichwa kwani ripoti ya MAPS ya 2025 inabainisha kuwa kuna ukosefu wa ripoti za kitakwimu zinazoweza kupakuliwa kwa urahisi ili kuonyesha thamani ya mikataba iliyochapishwa kwa kila mamlaka kwa mwaka husika.

Ingawa mamlaka zinatakiwa kutumia asilimia 70 ya bajeti kwa ajili ya manunuzi, ripoti za ukaguzi za miaka ya nyuma 2021/22 zinaonyesha kuwa ni taasisi chache zilizoweza kutekeleza mpango wao wa manunuzi kwa zaidi ya asilimia 50.

Ripoti hiyo ya MAPS inaeleza kuwa thamani ya jumla ya manunuzi ya umma nchini kwa mwaka 2025, inatarajiwa kuwa shilingi trilioni 30.12 kama ilivyoainishwa kwenye mipango ya manunuzi (APP) iliyopo kwenye NeST.

Hii inamaanisha kuwa kama sheria ingefuatwa basi makundi maalum yangetengewa zaidi ya shilingi trilioni 9 kutoka kwenye manunuzi hayo.

**Idadi ya wazabuni kwenye NeST**

Hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya kampuni 19,300 zilikuwa zimejisajili kwenye mfumo huo.

Kati ya hizo, asilimia 96 ya kampuni ni za soko la ndani, lakini mgawanyo wa idadi ya makundi maalum haukuainishwa moja kwa moja katika takwimu hizo.

**Waliofanikiwa**

Kulingana na vyanzo vilivyotolewa, hakuna idadi moja ya jumla ya kitaifa inayotaja idadi kamili ya makundi maalum yaliyofanikiwa kupata zabuni nchi nzima kwa mwaka 2024/25.

Hata hivyo, takwimu za ukaguzi na tafiti za hivi karibuni zinaonyesha kuwa waliofanikiwa kupata zabuni hizo ni idadi ndogo sana kutokana na kutokutekelezwa kwa takwa la kisheria la kutenga asilimia 30 ya bajeti kwa makundi hayo.

Malengo ya serikali

Serikali kupitia mpango wa MAPS na Benki ya Dunia (WB), imeweka malengo ya kuhakikisha angalau asilimia 5 ya thamani ya mikataba yote inayotolewa kupitia NeST inakwenda kwenye biashara zinazomilikiwa na wanawake ifikapo mwaka 2028.

Malengo mengine ni kuongeza idadi ya wazabuni wa ndani waliosajiliwa kwenye mfumo wa NeST ambao hadi Aprili 2024 walikuwa wamefikia 19,300.

**Mapendekezo**

Ripoti ya MAPS ya mwaka 2025 imeainisha kuwa ili kuboresha ushiriki wa makundi maalum, PPRA iendelee kutoa mafunzo kwa mamlaka nunuzi na wazabuni hasa biashara zinazomilikiwa na wanawake kuhusu mahitaji ya kisheria.

Pia inapendekeza uboreshaji wa mfumo wa NeST kwa kutengeneza "Dirisha la Manunuzi" ndani ya mfumo wa NeST ili kuwezesha ufuatiliaji wa takwimu na utekelezaji kwa urahisi.

Pendekezo jingine ni PPRA kufuatilia kupitia ukaguzi wa kila mwaka ili kuhakikisha mamlaka nunuzi zinatekeleza takwa hilo kwa vitendo na si kwa nadharia tu.

(Fuatilia toleo lijalo ili kujua mamlaka zinasema nini kuhusiana na suala hili ambalo linawaathiri wajasiriamali wengi wadogo wadogo nchini).

■ Habari

# Samia: Tukosoeni kwa heshima



Rais Samia Suluhu Hassan

Na Mwandishi WETU, Dodoma

RAIS Samia Suluhu Hassan amezitaka nchi ambazo hazikubaliani na jinsi serikali ilivyoshughulikia ghasia za uchaguzi mkuu mwaka jana kwa kutumia nguvu kubwa, kukosoa huku zikitilia maanani kuwa Tanzania ni nchi huru.

Akihutubia kusanyiko la mabalozi na wanadiplomasia katika Ikulu ya Chamwino, Dodoma wiki iliyopita, Rais Samia amesema serikali ililazimika kufanya kile ilichofanya siku ya Oktoba 29 mwaka jana na siku chache baadaye "ili kulinda usalama wa nchi na wananchi wake mkiwemo ninyi."

Hii ni mara ya kwanza kwa mkutano kama huo kufanyika katika Ikulu ya Chamwino.

Katika hotuba yake, Rais Samia alikiri kuwa tukio hilo limeitia doa kubwa nchi, lakini akaahidi kuwa serikali itafanya kila linalohitajika ili kuhakikisha kuwa hali kama hiyo haijirudii tena.

Ili kukabiliana na ghasia hizo, serikali ilichukua hatua kadhaa ikiwamo kuzima mtandao wa intaneti na kuzuia watu kutoka majumbani.

Katika siku ambazo watu walikaa majumbani, askari walikuwa wakifanya doria mitaani na inaelezwa kuwa watu wengi waliuawa kipindi hicho.

Katika hotuba yake kwa mabalozi, Rais Samia alibainisha kuwa baada ya tukio hilo, serikali ilipokea salamu nyingi za pole kutoka kwa nchi, taasisi na watu mbalimbali.

"Wale waliotutumia salamu za pole kupitia njia sahihi za kidiplomasia tunawaambia kuwa tumepokea salamu zao, lakini wapo ambao hawakututumia salamu zozote, lakini nao tunawaambia kuwa ujumbe wao umetufikia…"

"Lakini tunapenda kuwafahamisha kuwa wanapoamua kutukosoa, basi wafanye hivyo wakizingatia kuwa Tanzania ni nchi huru," alisema.

Ingawa Rais Samia hakuzitaka balozi au taasisi, lakini rekodi zinaonyesha kuwa zipo baadhi ya balozi na taasisi za kimataifa zilitoa taarifa zikikosoa namna serikali ilivyoshughulikia ghasia za Oktoba 29 mwaka jana zilizosababisha vifo, majeruhi na uharibifu mkubwa wa mali na miundombinu.

Pamoja na masuala hayo ya kisiasa, Rais Samia pia alitumia kusanyiko hilo kuelezea mipango ya kiuchumi ambayo utekelezaji wake tayari umeshaanza kupaisha uchumi katika mwelekeo wa kuifanya Tanzania kuwa moja ya nchi zenye uchumi imara Afrika.

Katika hotuba hiyo, Rais Samia alibainisha kuwa Tanzania imejipanga kutumia rasilimali ilizonazo, uhusiano wa kimataifa, vijana ambao ndiyo nguvu kazi kubwa na kuimarika kwa biashara nchini na duniani kama sehemu ya mambo yatakayotumika kuipaisha nchi kiuchumi.

Alisema lengo kubwa ni kuhakikisha Tanzania inakuwa na uhuru wa kiuchumi, unaotokana na utakaowawezesha wananchi kuendesha shughuli zao kwa ufanisi, ujenzi wa miundombinu imara ya viwanda, na ushirikiano wa kimkakati.

Lengo, alisema, ni kuhakikisha kuwa uchumi unakua kwa kiwango cha tarakimu mbili kutoka kwenye kasi ya hivi sasa.

Kwa miaka mingi ya karibuni uchumi wa Tanzania umekuwa ukikua kwa kati ya asilimia 5 na 6, lakini chini ya utekelezaji wa Dira 2050 nchi inalenga kujenga uchumi imara zaidi wenye thamani ya dola trilioni moja za Kimarekani ifikapo mwaka 2050.

Inaendelea Uk. 16-17

# Samia: Tukosoeni...

Inatoka Uk. 16

Alisema Dira 2050 ndiyo itakayotoa mwongozo kupitia diplomasia ya uchumi, akisisitiza kufungua fursa za sekta binafsi, kuvutia uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje (FDI), na kupanua sekta zinazozalisha ajira na kuongeza thamani ya mazao na rasilimali, mambo ambayo tayari yameshaanza kufanyika na kuonyeha matokeo mazuri.

"Ujumbe wetu uko wazi, Tanzania inaondoka katika kuuza malighafi na kuelekea kuuza bidhaa zilizoongezwa thamani," alisema, akibainisha kuwa utulivu wa kiuchumi, kutabirika kwa sera na mageuzi ya kisheria, vitaendelea kuwa nguzo za ushirikiano wa Tanzania na washirika wa kimataifa.

**Uchumi imara, imani inaongezeka**

Aliwaambia wanadiplomasia hao kuwa Tanzania inaendelea kuwa miongoni mwa nchi zinazokua kwa kasi zaidi Afrika, ikirekodi ukuaji wa Pato la Taifa (GDP) wa asilimia 5.9 huku mfumuko wa bei ukiendelea kuwa thabiti katika kiwango cha asilimia 3.3.

Alibainisha kuwa dalili njema zimeanza kuonekana kutokana na hatua zilizochukuliwa na serikali kwani katika mwaka uliopita idadi ya miradi ya uwekezaji kutoka nje ya nchi imeongezeka kwa kasi ya ajabu.

Aidha, kumekuwepo kwa kuongezeka kwa imani ya wawekezaji kunaonekana kupitia matokeo mazuri ya utafiti uliofanywa na kampuni za kimataifa za Moody na Fitch kuhusu uwezo wa nchi kukopesheka.

Akifafanua, alisema katika utafiti wake, Moody iliipa Tanzania alama B1 huku Fitch ikitoa alama ya B+, ambazo ni alama za juu.

Alibainisha kuwa mtaji wa soko katika Soko la Hisa la Dar es Salaam uliongezeka kwa zaidi ya asilimia 34 mwaka 2025 na kufikia karibu shilingi trilioni 24, ikiwa ni dalili nzuri ya nchi kuvutia uwekezaji kutoka ndani na nje ya nchi.

"Imani hiyo imezaa matunda kupitia usajili wa miradi mipya ya uwekezaji 927 kufikia Desemba 2025, yenye thamani ya zaidi ya dola za Marekani bilioni 11 – ikiwa ni idadi kubwa zaidi tangu kuanzishwa kwa Kituo cha Maeneo Maalum ya Biashara na Uwekezaji Tanzania (TISEZA)," libainisha.

Miradi hiyo inatarajiwa kuzalisha zaidi ya ajira 162,000, huku wawekezaji wa ndani wakichangia takribani theluthi moja ya miradi yote.

"Kwa wawekezaji wetu, tunaahidi kuwa uwekezaji uliopo na mpya utalindwa," alisema Rais Samia.

Kutoka ukuaji kwenda mageuzi ya kimuundo Rais Samia alibainisha kuwa matokeo hayo mazuri yanayoonekana kupitia takwimu ni matokeo ya mageuzi ya muundo wa uendeshaji wa uchumi.

Alibainisha kuwa sekta ya kilimo inaendelea kuwa mhimili wa usalama wa chakula, huku Tanzania ikirekodi uwiano wa kujitosheleza kwa chakula wa asilimia 128.

Kwa upande mwingine, sekta ya madini imeibuka kuwa kichocheo kikuu cha ukuaji uzalishaji wa madini ukiwa umeongezeka kwa zaidi ya asilimia 48 mwaka wa fedha 2024/25.

Ili kuimarisha uimara wa uchumi, serikali sasa imewataka wachimbaji wakubwa wa dhahabu kuuza angalau asilimia 20 ya dhahabu wanayozalisha kwa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), hatua inayoongeza akiba ya fedha za kigeni.

Ripoti za BoT zinaonyesha kuwa hadi mwishoni mwa mwaka jana ilikuwa imekusanya kiasi cha tani 15.37 za dhahabu kupitia mpango wake wa ununuzi wa madini hayo, ikiwa ni hatua muhimu ya kuongeza akiba ya fedha za kigeni na kuimarisha thamani ya shilingi.

Kwa mujibu wa rais Samia, sekta ya utalii pia imeleta mapinduzi makubwa kwani mapato ya utalii yakifikia karibu dola bilioni 4 kufikia robo ya tatu ya mwaka 2025.

Alisema kutambuliwa kwa Tanzania kama Kituo Bora cha Safari Duniani katika Tuzo za Utalii Duniani (World Travel Awards) kumeimarisha taswira ya nchi kimataifa, huku upanuzi wa safari za Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL) ukichochea biashara, utalii na muunganiko wa kikanda.

# Benki Kuu yageuka kituo cha mafunzo kimataifa

**Na Mwandishi WETU**

Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imegeuka kuwa kituo kikubwa cha mafunzo kwa benki kuu nyingine kutoka Afrika.

Jarida la Uchumi, linalochapishwa na BoT limebainisha kuwa katika kipindi kifupi kilichopita, maofisa kutoka benki kuu za Shelisheli na Rwanda wamepata mafunzo kupitia BoT.

Kwa mujibu wa maofisa wa BoT hali hiyo inatokana na umahiri ambao BoT imeuonyesha katika uendeshaji wa shughuli zake.

Jarida hilo linaeleza kuwa wataalamu mbalimbali kutoka Benki Kuu ya Shelisheli (CBS) walitembelea BoT kwa ajili ya kujifunza jinsi inavyotengeneza na kuendesha mifumo yake ya Tehama kwa kutumia wataalamu wa ndani ya taasisi.

Ziara hiyo ilifanyika Novemba mwaka jana katika ofisi za BoT jijini Dar es Salaam.

Katika ziara hiyo, wataalamu hao walipatiwa muhtasari wa namna BoT inavyotengeneza na kuendesha mifumo yake, taratibu za uhakiki wa ubora, pamoja na hatua zinazochukuliwa kuhakikisha usalama wa mifumo hiyo.

Aidha, walielimishwa kuhusu mchakato uliotumika katika utengenezaji wa Mfumo wa Malipo ya Papo kwa Hapo (TIPS) pamoja na Mfumo Mkuu Jumuishi wa Kibenki (iCBS), yote ikiwa ni mifumo iliyotengenezwa na wataalamu wa ndani ya taaisisi.

Pia, wataalamu hao kutoka Shelisheli walipata fursa ya kutembelea Makumbusho ya BoT, ambapo walielezwa kuhusu historia ya fedha nchini, pamoja na historia ya benki hiyo tangu kuanzishwa kwake Juni 14, 1966.

Akizungumza baada ya kutembelea makumbusho hayo, mmoja wa wataalamu kutoka CBS aliipongeza BoT kwa kuanzisha makumbusho yake yenye maudhui ya kina yanayoelezea historia ya maendeleo ya uchumi na sekta ya fedha nchini kwa muktadha wa tulipotoka, tulipo na tunapoelekea.

**Rwanda nao watembelea**

Katika kuhakikisha kuwa BoT inakuwa kitovu cha maarifa na uga wa kujifunza ilitembelewa pia na wataalamu kutoka Benki Kuu ya Rwanda (BNR).

Wataalamu hao walitembelea BoT kwa ajili ya kujifunza jinsi inavyotengeneza na kuendesha mifumo ya Tehama kwa kutumia wataalamu wa ndani ya taasisi na kubadilishana uzoefu.

Wataalamu hao walijifunza kuhusu mbinu bora zilizosaidia Benki Kuu ya Tanzania kufanikisha matumizi ya mifumo ya kidijitali, pamoja na mikakati ya kuimarisha ufanisi wa mifumo ya usimamizi wa nyaraka katika taasisi za kifedha.

Aidha, walijifunza namna BoT inavyotengeneza na kuendesha mifumo yake, taratibu za uhakiki wa ubora, pamoja na hatua zinazochukuliwa kuhakikisha usalama wa mifumo hiyo.

Vilevile, walieleza kuridhishwa kwao na maarifa waliyopata, wakisema kuwa uzoefu huo utasaidia kwa kiasi kikubwa katika maboresho ya mifumo yao.

Ziara hiyo ilihitimishwa kwa pande zote mbili kuahidi kuendelea kushirikiana katika masuala ya teknolojia na mifumo, ikiwa ni hatua muhimu ya kuimarisha ushirikiano wa kikanda katika sekta ya fedha.



# REA yaingia kwenye miradi mikubwa

Na Mwandishi WETU

SERIKALI kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) imezindua kituo cha kupoza na kusambaza umeme cha Mtera na kusaini mikataba ya kutekeleza mradi kabambe wa kusambaza umeme kwenye vitongoji 9,009 katika mikoa yote Tanzania Bara.

Akizungumza jijini Dodoma wiki iliyopita, Mkurugenzi Mkuu wa REA, Mhandisi Hassan Saidy, amesema huo ni mmoja wa miradi mikubwa ya nishati ambayo REA imepanga kujihusisha nayo.

Mradi huo umezinduliwa na Waziri wa Nishati, Deogratius Ndejembi (pichani).

Kituo cha kupoza umeme cha Mtera kilizinduliwa Ijumaa iliyopita ambapo pia ilisainiwa mikataba 30 yenye thamani ya shilingi trilioni 1.2 kwa ajili ya kutekeleza mradi mkubwa wa kusambaza umeme katika vitongoji zaidi ya 9,000 nchini.

Kituo hicho cha kupoza umeme kimejengwa kwa gharama ya shilingi bilioni 9.2 na serikali kupitia REA kwa ushirikiano na serikali za Sweden na Norway.

Aidha, Mhandisi Saidy amesema mikataba hiyo iliyosainiwa itahusisha wakandarasi 21 wazawa na wakandarasi tisa kutoka nje ya nchi, lakini wamesajiliwa nchini kwa ajili ya kutekeleza mradi huo utakaotekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu nchi nzima.

Amewataka wananchi kuchangamkia fursa zitakazopatikana wakati wote wa utekelezaji wa miradi hiyo ikiwemo ajira, biashara na huduma mbalimbali zitakazohitajika.

Lakini kubwa zaidi, Mhandisi Saidy aliwataka wananchi kujiweka tayari kwa ajili ya kutumia umeme utakaopatikana kupitia miradi hiyo akibainisha kuwa iwapo umeme huo hautatumika kwa ajili ya uzalishaji basi miradi hiyo itapoteza maana yake.

Alisema ni vyema wananchi wakazitumia fursa hizo zinazotengenezwa na serikali kuongeza uzalishaji kupitia ujasiriamali.

"Hivi sasa nishati si tatizo tena nchini katika uzalishaji. Serikali kupitia miradi kama hii imehakikisha kuwa nishati inamfikia kila mzalishaji. Ni wakati wa Watanzania sasa kujikita katika uzalishaji mali," alisema.



Alisema pamoja na ujasiriamali, miradi hiyo pia itasaidia kuimarisha na kusambaza huduma za jamii katika sekta za elimu, maji na afya.

"Tunatekeleza maono ya Rais Samia Suluhu Hassan. Mradi huu unakwenda kufungua nchi kiuchumi ni wa kipekee na mradi mkubwa kuwahi kutekelezwa na REA kwa viwango vya gharama na idadi ya vitongoji vitakavyofikiwa," amesema.

**Miradi ya REA**

REA inaendelea kuwa mhimili muhimu katika upanuzi wa upatikanaji wa umeme na huduma za nishati safi nchini, hatua inayochochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika maeneo ya vijijini.

Hadi hivi sasa, kupitia REA serikali imefanikiwa kuunganisha zaidi ya vijiji 12,000 vya Tanzania Bara kwenye gridi ya taifa, na kuweka msingi wa kufikia umeme kwa karibu vijiji vyote nchini.

Juhudi sasa zinaelekezwa katika kuunganisha vitongoji, ambapo zaidi ya vitongoji 39,000 kati ya 64,359 tayari vimepata umeme, huku lengo likiwa ni kufikia asilimia 100 ifikapo mwaka 2030.

Maendeleo makubwa yameripotiwa katika mikoa kama Arusha na Tanga, ambayo imefikia asilimia 100 ya uunganishaji wa vijiji kwenye umeme. Hata hivyo, Serikali imesisitiza umuhimu wa kuongeza kasi ya uunganishaji wa kaya ili wananchi wanufaike kikamilifu na miundombinu iliyowekwa.

Habari




*Waziri Mkuu Dkt. Mwigulu Nchemba*

# Wadau wazungumza ahadi siku 100 za Rais Samia

Na Mwandishi WETU

WAHENGA wanasema ahadi ni deni na sasa baadhi ya wananchi wameanza mjadala kuhusu utekelezaji wa ahadi ambazo serikali iliahidi kuzitekeleza ndani ya siku 100 baada ya kuingia madarakani Novemba mwaka jana, 2025.

Katika hotuba yake baada ya kuapishwa Novemba 3, mwaka jana, Rais Samia Suluhu Hassan aliorodhesha baadhi ya mambo ambayo alisema yatatekelezwa katika kipindi cha siku 100 za kwanza za uongozi wake.

Zikiwa zimebaki takriban wiki mbili kufikisha siku 100 zilizoahidiwa, baadhi ya wananchi wameelezea wasiwasi wao kuhusu utekelezaji kwani mpaka sasa hakuna taarifa rasmi iliyotolewa kuonyesha kilichofanyika katika kutekeleza ahadi hizo.

Hata hivyo, katika mahojiano ya gazeti hili baadhi ya wananchi wamesema wanaridhishwa na utendaji kazi wa Rais Samia, kwani katika kipindi kifupi amefanya mambo mengi yakiwamo ambayo siyo sehemu ya mambo yaliyoahidiwa kutekelezwa katika siku 100.

Baadhi ya mambo ambayo Rais Samia aliahidi kutekeleza katika siku 100 ni pamoja na kuanzishwa kwa Bima ya Afya kwa Wote, serikali kuanza utaratibu wa kuhudumia wagonjwa wa magonjwa yasiyoambukiza, kuzua tabia ya hospitali kuzuia miili ya wanaodaiwa ankara za matibabu na kuanzisha mchakato wa maridhiano ikiwamo kufufua mchakato wa kuandikwa kwa Katiba Mpya.

Katibu Mkuu wa Shura ya Maimamu nchini, Sheikh Ponda Issa Ponda, amesema kuna umuhimu mkubwa kufufua mchakato wa kuandika Katiba Mpya.

"Rais aliahidi mambo kadhaa ndani ya siku 100 za kuwapo madarakani, walau angetekeleza mambo machache kati ya aliyoahidi ikiwamo kuanza mchakato wa Katiba Mpya..."

"Inatia wasiwasi kidogo kuwa imetangazwa kuwa mchakato huo utachelewa kidogo kupisha suala la maridhiano," amesema.

Sheikh Ponda amesema ni vyema kuandikwa kwa Katiba Mpya kukapewa kipaumbele kwani hiyo ndiyo dira ambayo itaiongoza nchi kutekeleza mambo mengine kama vile maridhiano.

Akifafanua, amesema kuwa maridhiano yatakuwa na maana kubwa iwapo yatafanyika chini ya mazingira ya Katiba Mpya ambayo inakubalika na kila mdau nchini.

Kwa upande wake, aliyewahi kuwa Mbunge wa Afrika Mashariki ambaye hakutaka jina lake litajwe gazetini, amesema jambo ambalo Rais Samia alipaswa kulifanyia kazi kwa haraka ni kuponya majeraha yaliyotokana na ghasia zilizotokea wakati na baada ya uchaguzi mkuu.

Inaendelea Uk. 21

# Wadau wazungumza...

Inatoka Uk. 20

"Kwa kuonyesha kuwa mambo siyo shwari kabla ya siku 100 kutimia, tumeshuhudia Baraza la Mawaziri limepanguliwa, hii maana yake ni kwamba ndani ya serikali yetu bado hakuko sawa huenda wao kwa wao hawaaminiani,"amesema.

Naye Mwenyekiti wa Jumuia ya Wazazi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Siha, Kilimanjaro, Mwalimu Meijo Laizer, amesema baada ya uchaguzi mkuu kumalizika taifa lina amani na utulivu na hilo ni jambo kubwa.

"Tunapoelekea siku 100 za Rais Samia na ahadi zake sisi wadau wa maendeleo tunaona upande wa ajira hasa kwenye sekta ya elimu zimetolewa na bado zinatolewa… zege halilali," amesema Laizer.

Kada huyo wa CCM amesisitiza umuhimu wa maridhiano na kueleza kuwa huondoa huzuni na kurejesha furaha, hujenga undugu pia daraja la kujenga taifa.

"Niwaombe Watanzania wenzangu tumpe ushirikiano Rais Samia ili azma yake ya maridhiano itimie. Lakini tufahamu kuwa mambo mengine yanahitaji muda, hivyo tuwape muda viongozi wetu wayafanyie hasa yale yanayohusu sera, sheria na yanayohitaji vyombo vya maamuzi kama vile bunge ili yapitishwe na kupitishwa," anasema.

Mwanasiasa, Joseph Selasini, amesema taifa linahitaji uponyaji ili ahadi alizoahidi Rais Samia zitekelezeke.

"Ninachokiona nchi iko kwenye sintofahamu baada ya uchaguzi mkuu, hadi sasa sijaona ahadi iliyotekelezwa zaidi ya maneno. Kama yupo mtu ataibuka na kudai kuna ahadi zimefanyika nitamshangaa sana hali ya nchi yetu haijapoa…"

"Tujifunze kupitia nchi za wenzetu, yanapoingia machafuko au ghasia zozote hakuna maendeleo yanayofanyika."

Mkazi wa Ubungo Maziwa, Dar es Salaam, Asia Feruz, amesema haoni umuhimu wa kuhesabu siku za Rais Samia kuwapo madarakani, badala yake maisha ya Watanzania yaboreshwe.

"Huku mitaani maisha ni magumu sana. Tunamuomba Rais Samia atuondolee huu ugumu, hata tukihesabu hizo siku haitusaidii chochote,"anasema Asia.

Daktari katika moja ya hospitali za rufaa jijini Dar es Salaam ambaye hakutaka jina lake kutajwa gazetini amesema; "Bado tunasubiri mpango wa huduma bure uanze kufanya kazi. "Tuliambiwa utaanza Januari 2, mwaka huu bila shaka kuna mambo yanaendelea kuwekwa sawa ili ahadi ya Rais iweze kutimia,"anasema.


Rais Samia aliahidi mambo 10 atakayoyafanya ndani ya siku 100 za utawala wake ikiwamo kuajiri wahudumu wa afya 5,000.

Aidha, serikali yake itagharamia vipimo na matibabu ya kibingwa kwa asilimia 100 kwa wasiojiweza kwenye magonjwa makuu ikiwamo saratani, figo, moyo, kisukari, mifupa na mishipa ya fahamu.

Rais Samia aliahidi kupiga marufuku kwa hospitali zote nchini kuzuia miili ya marehemu kuchukuliwa na ndugu zao kutokana na kudaiwa fedha za huduma aliyopewa wakati akiwa hai.

Miongoni mwa mambo ambayo yamekuwa yakizungumziwa sana hususan na upinzani ni kurejeshwa kwa mchakato wa katiba mpya, hivyo rais aliahidi kuwa ndani ya siku 100 serikali yake itaandaa mazingira ya kuanza mchakato wa Katiba mpya.

Hivi karibuni Waziri Mkuu Dkt. Mwigulu Nchemba alizungumzia utekelezaji wa ahadi hizo na kueleza kuwa Rais Samia amekwishatoa ajira kwa wataalamu 5,000 wa sekta ya afya na walimu wa sekta ya elimu 7,000.



# WHO: Tanzania inachangia asilimia nne ya vifo vya malaria duniani

Na Mwandishi WETU

TANZANIA imetajwa miongoni mwa nchi zilizoathirika zaidi na ugonjwa wa malaria, ikichangia takriban asilimia nne ya vifo vyote vya malaria duniani.

Ripoti ya Malaria Duniani kwa mwaka 2025 iliyotolewa na Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO) inaeleza.

Ripoti hiyo inaiweka Tanzania miongoni mwa nchi nne za Afrika - pamoja na Nigeria, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) na Niger - ambazo kwa pamoja zinachangia zaidi ya asilimia 50 ya vifo vyote vinavyohusiana na malaria duniani.

**Ukubwa wa tatizo duniani**

WHO inaripoti kuwa mzigo wa malaria duniani bado ni mkubwa sana. Mnamo 2024, jumla ya watu milioni 282 waliugua ugonjwa huo, huku vifo vikifikia 610,000 duniani kote, ikionesha kuongezeka kwa maambukizi na vifo baada ya miaka kadhaa ya kupungua kwa idadi ya wagonjwa.

Kanda ya Afrika ya WHO inachangia takriban asilimia 94 ya maambukizi yote ya malaria duniani na asilimia 95 ya vifo vyote.

Watoto chini ya miaka mitano bado ndilo kundi linalooathirika zaidi, likiwakilisha idadi kubwa ya vifo vya malaria barani Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Aidha, WHO inabainisha kuwa hali hii inaonesha upungufu mkubwa katika hatua za kinga, uchunguzi wa mapema pamoja na upatikanaji wa matibabu stahiki, na kusisitiza kwamba ili kupunguza athari za malaria kwa kundi hili ni muhimu sana kwa afya ya umma na maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa ujumla.
Hali halisi Tanzania

Kwa mujibu wa ripoti hiyo iliyotolewa mwishoni mwa mwaka jana, maambukizi ya malaria nchini bado ni makubwa.

Takribani asilimia 93 ya wananchi wanaishi katika maeneo yenye malaria, jambo linalofanya ugonjwa huo kuenea sehemu kubwa ya nchi na kuwa mgumu kudhibiti.

Wataalamu wanasema sababu kadhaa zinachangia malaria kuendelea kuwa mzigo mkubwa nchini, ikiwemo kuendelea kuongezeka kwa kasi kwa idadi ya watu, mabadiliko ya tabia nchi, ukosefu wa huduma za afya maeneo ya vijijini, na bajeti finyu za kufadhili mipango ya kuzuia malaria.

**WHO yaonya**

Mkurugenzi Mkuu wa WHO, Dkt. Tedros Adhanom Ghebreyesus, anasema kuwa pamoja na jitihada za miaka mingi za kupambana na malaria bado kuna kazi kubwa ya ziada ya kufanya ili kukabiliana na ugonjwa huo kikamilifu.

“Mbinu mpya za kuzuia malaria zinatupa matumaini mapya, lakini bado tunakabiliana na changamoto kubwa. Kuongezeka kwa maambukizi na vifo, tishio la usugu wa dawa, na kupunguzwa kwa fedha zinazohitajika kupambana na ugonjwa huu, kunatishia kuvuruga mafanikio tuliyoyapata katika miongo miwili iliyopita,” anasema Dkt. Tedros.

Ripoti hii mpya inaonesha kuwa Tanzania ilirekodi takriban maambukizi 3.8 milioni za malaria na vifo 25,500 mnamo 2023. Ingawa idadi hii ni ndogo ikilinganishwa na vifo takriban 44,280 mwanzoni mwa miaka ya 2000, limekuwepo ongezeko kidogo la vifo katika miaka sita iliyopita.

Kiwango cha vifo vya malaria nchini sasa ni takriban watu 2.2 kwa kila watu 100,000, kinachotokana na ugunduzi bora wa maambukizi, upatikanaji mpana wa matibabu, na uboreshaji wa huduma za afya.



Tunakaribisha barua. Tuma kupitia

Tuandikie kero ya eneo lako kupitia WhatsApp namba;
+255 712 792216 au tutumie kupitia email; info@pambazuko.or.tz

## Nani wanufaika wa mikopo ya halmashauri?

**Mhariri,**

MIMI ni miongoni mwa wanawake wajasiriamali ambao tuliwahi kujiandikisha katika Kata ya Sinza, Ubungo, Dar es Salaam, ili tuweze kunufaika na mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na halmashauri.

Pamoja na kwamba tulihangaika huku na kule ili kukamilisha masharti yote, lakini hadi leo ni miaka kumi hatujaona dalili ya kupata mikopo hiyo.

Tunajiuliza mikopo hii wanapewa kina nani na kwanini itolewe kwa ubaguzi?

**Leila Ahmed,**
**Sinza, Dar es Salaam.**

## Tunateseka ubovu barabara kuelekea Hospitali ya Wilaya Karatu

**Mhariri,**

NALETA kero tunayoipata kuhusu changamoto ya miundombinu ya barabara ya kuelekea hospitali yetu ya Wilaya ya Karatu.

Kama inavyofahamika, aina ya udongo wa Karatu wakati wa mvua huzalisha tope zito ambalo hukwamisha upitaji, iwe kwa gari na hata kwa miguu.

Unapokuwa na mgonjwa hata kama una gari la kubebea wagonjwa, mvua ikinyesha huwezi kufika hospitalini kwa sababu pia kuna daraja linalojaza maji, ambalo halipitiki wakati wa masika.

Kutokana na hali hiyo, na kuepusha kutokea kwa vifo, tunaomba tujengewe barabara ya kiwango cha lami kuanzia Njiapanda kuelekea Hospitali ya Wilaya ya Karatu.

**Novline Hhayuma,**
**Bashay, Karatu.**

## Nini umuhimu wa NHIF kama dawa tunalipia?

**Mhariri,**

TUNASHANGAZWA na utaratibu wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), kwamba pamoja na kuwa mgonjwa ana kadi, lakini mara nyingi baadhi ya vipimo na dawa anaambiwa alipie.

Kwa mfano, mama yangu mzazi anatumia bima ambayo analipia 708,000 kwa mwaka, lakini mara nyingi akienda hospitali kufanya vipimo vya miguu na damu anaambiwa alipie dawa, tena zingine ni zile za kutuliza maumivu.

Nadhani NHIF wangeweka utaratibu mzuri wa kuwa wa wazi pale mwanachama anapojiunga aambiwe kabisa kwamba kifurushi fulani lazima alipie dawa.

Zaidi ya hapo, kwa maoni yangu, sioni umuhimu wa kuwa na bima kama mwanachama anayelipia kifurushi cha 708,000 analipia hadi dawa za maumivu.

**Lucyta Jackson**
**Majengo, Moshi.**



## Kilinge cha Mawasiliano

Na Loth MAKUZA

# Uhusiano wa umma Tanzania kubadilika au kufifia?

MIEZI michache iliyopita, wakati nazungumza na wenzangu kwenye sekta; swali moja liliendelea kujirudia kimyakimya; je, tuko tayari kwa kile ambacho mwaka 2026 unaleta mabadiliko katika Sekta ya Uhusiano wa Umma nchini Tanzania, siyo kwa kaulimbiu tu, bali kwa vitendo?

Tafiti mbalimbali zimejaribu kujibu swali hilo. Takribani wataalamu 600 wa uhusiano na umma na mawasiliano, waliulizwa mustakabali unaonekanaje. Majibu hayashangazi, lakini yanatia shaka kwamba kuna pengo, tena kubwa katika kujibu swali hilo.

Uongozi unaamini kuwepo kwa watendaji wasiokuwa wepesi kubaini na kuchukua hatua ili kuendelea kuwepo na kushamiri kwa sekta.

Wapo wanaoamini kuwa mabadiliko ya nyakati na sayansi, hayapaswi kubadilisha taratibu za mawasiliano kwa haraka.

Pia, wengine wanadhani kuwa mabadiliko ya teknolojia ni muhimu kwenda sambamba na mabadiliko ya fikra na uamuzi katika utendaji wa sekta hiyo.

Hawa wanajikita zaidi katika mazingira ya kuwa na timu ndogo za watendaji zikibeba majukumu makubwa.

Akili mnemba (AI), uhalisia, na ulinganifu siyo maneno ya kuvutia tena. Ndio mazingira halisi ya kazi. Akili mnemba ni fursa kubwa zaidi inayokuja kwenye sekta.

Matumizi ya zana za kizazi cha maudhui, uchambuzi wa takwimu na kutumia sayansi kufanya kazi haraka na kwa ufanisi zaidi ndiyo mwendo wa sasa.

Lakini huu ndio ukweli ambao wengi hawapendi kuusikia; teknolojia haitaokoa fikra mbovu.

Hata kadri AI inavyozidi kuwa na nguvu, rasilimali zenye thamani zaidi katika PR bado ni za kibinadamu — ubunifu, uhusiano, uamuzi, na uaminifu. Ieleweke kuwa waandishi wa habari bado hujibu watu, hadhira bado huamini taarifa ndiyo maana watendaji wa PR wenyewe wanapanga vipaumbele vyao kwa umakini.

AI inakuja kwanza lakini nyuma yake ni uhusiano na waandishi wa habari, ushirikiano na waundaji wa maudhui na ulinganifu wa karibu na mkakati wa biashara. Huu siyo mgongano. Ni mizani.

Kwamba kwa sasa zana zinabadilika, lakini ujuzi unabaki.

Katika miaka ya hivi karibuni, wataalamu wa sekta wamekuwa wakijaribu matumizi ya AI, mara nyingi kwa udadisi, wakati mwingine kwa hofu.

Mwaka 2026 utakuwa tofauti. Huu ni mwaka ambapo majaribio yanaisha na nidhamu inaanza. AI itahama kutoka kuwa kitu cha majaribio kwenda kuwa sehemu ya mtiririko wa kazi.

Kutoka msisimko kwenda uwajibikaji. Wale wanaoendelea “kujaribu jaribu” wataachwa nyuma.

Lakini pengine mabadiliko makubwa zaidi yanafanyika kimyakimya katika mawasiliano ya migogoro.

Kufuatilia tu kutajwa hakutoshi tena. Alama za hisia pekee haziwezi kulinda chapa (brand). Taarifa potofu zinazoendeshwa na AI, na mitandao iliyoratibiwa ya roboti — vitisho hivi vinaenda kasi kuliko mifumo ya jadi ya majibu ya sekta.

Wataalamu wa sekta kwa sasa lazima walinganishe mikakati na utekelezaji wake kwa kuzingiatia mabadiliko ya sayansi na teknolojia. Nao viongozi lazima waondoe vikwazo badala ya kusherehekea wepesi ambao haupo.

AI lazima ikumbatiwe kwa makusudi, siyo kwa upofu. Takwimu na usimulizi wa taarifa lazima vikue pamoja. Na juu ya yote, uhusiano wa kibinadamu lazima yaendelee kuwa kiini.

AI haitachukua nafasi wataalamu wa sekta. Itaweka wazi walio dhaifu na kuwawezesha zaidi wale walio makini. Itawazawadia wale wanaofikiri kimkakati, wanaotenda haraka, na wanaweka taarifa kweli kwenye uhalisia.

Mwaka 2026, wataalam wa sekta sasa wana moja kati ya haya; kubadilika au kufifia kimyakimya kwa ukijifanya hakuna kilichobadilika.

# Gen Z ‘wanavyoihenyesha’ serikali



**Na Mwandishi WETU**

UTHUBUTU wa vijana wa kizazi kipya maarufu kama Gen Z kupanga maandamano ya amani yasiyokoma, kumeiweka nchi katika hali ya tahadhari kubwa.

Baada ya ghasia za Oktoba 29 mwaka jana, kila mara vijana hao wanapojitokeza na kutangaza maandamano, serikali imekuwa ikitumia nguvu kubwa kudhibiti maandamano hayo yasifanyike.

Hali hiyo imeshuhudiwa kila mara vijana hao wanapotangaza kufanya maandamano kiasi cha hivi sasa umegeuka kuwa “mchezo wa paka na panya.”

Baada ya Oktoba 29, vijana hao walitangaza kufanya maandamano Desemba 9, siku ya Sherehe za Uhuru wa Tanganyika na Desemba 25, siku ya Sikukuu ya Krismas.

Katika siku hizo zote, serikali ililazimika kuongeza ulinzi ukihusisha Jeshi la Polisi na Jeshi la Wananchi (JWTZ).

Na siyo siku hizo tu kwani tahadhari kama hiyo imeshuhudia hata katika siku ambazo vijana hao hawajatangaza kufanya maandamano, lakini zikiwa ni siku za mapumziko kitaifa ikiwamo Desemba 31 siku ya mkesha wa mwaka mpya na Januari 12, siku ya sherehe za Mapinduzi ya Zanzibar, hali ya kuimarishwa ulinzi kama tahadhari ya maandamano ya Gen Z ilishuhudiwa.

Imeshuhudiwa kuwa katika siku ambazo vijana hao walitangaza kuandamana, serikali imekuwa ikikusanya majeshi ya ulinzi na usalama kuhakikisha kuwa hilo halitokei. Kwa mtu ambaye ni mgeni aliyetembelea Dar es Salaam siku hizo angeweza kudhani kuwa nchi ipo katika hali ya hatari, lakini kumbe ni kudhibiti Gen Z kuandamana.

Tangu maandamano ya Oktoba 29, 2025, nchi imeshuhudia siku 81 zenye kitendawili kikubwa kwani bado Gen Z wana kiu ya kutimiza azma yao ya kuandamana.

Kwanza walitangaza kuandamana siku ya sherehe za Uhuru wa Tanganyika – Desemba 9 mwaka jana. Siku hiyo tukashuhudia kuimarishwa kwa ulinzi mitaani ukihusisha jeshi la Polisi na Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), ambalo ni nadra sana kushiriki shughuli za usalama wa raia na mali zao ndani ya nchi.

Kwa kawaida JWTZ lina jukumu la kuilinda nchi dhidi ya maadui wa nje.

Ni Dhahiri kuwa rasilimali za nchi kama vile magari maalum ya kijeshi, silaha, muda na rasilimali nyingine nyingi zinatumika kwa ajili ya udhibiti huo kwa tishio hilo la Gen Z.

Matishio ya vijana hao ni dhahiri kuwa yameyafanya majeshi ya ulinzi kuwa macho wakati wote wakilinda nchi kwa juhudi na maarifa makubwa ili kuhakikisha kuwa vijana hao hawafanikiwi katika azma yao hiyo.

Katika maeneo mengi jijini Dar es Salaam, hasa maeneo nyeti na makutano ya barabara kuu kama Tazara, Veta, Misheni (Barabara ya Kilwa), Mwenge, Sayansi (Barabara ya Bagamoyo) na maeneo mengine kila mara yameendelea kushuhudia ulinzi mkali kila vijana hao wanapotoa trishio la kuandamana.

Inaendelea Uk. 26

## Makala



# Gen Z 'wanavyoihenyesha'...

Inatoka Uk. 25

Askari wa Jeshi la Polisi na wale wa JWTZ (kutokana na sare zao) wanaonekana wakiwa katika magari maalumu ya ulinzi wakiwa wameshikilia silaha za kivita.

Maeneo mengine ambayo ulinzi umeimarishwa kwa kiasi kikubwa ni katika vituo kadhaa vya Mwendokasi, maeneo ya Tabata, Mbezi, Ubungo na mengine huku askari wanaolinda maeneo hayo wakiwa na silaha na vifaa vingine vya ulinzi yakiwemo mabomu ya machozi.

Lakini pia wakati wa uchaguzi na kabla ya kuhesabiwa kwa kura na mshindi kutangazwa huduma za intaneti zilikatishwa kwa siku tatu nchini hivyo kusababisha athari na usumbufu mkubwa kutokana na kukosekana kwa mawasiliano.

Hali hiyo ilisababisha pia wananachi kutangaziwa kubaki majumbani ili kupisha hali ya utulivu na amani katika maeneo mbalimbali.

Wiki iliyopita katika hotuba yake kwa mabalozi walioko nchini Tanzania, Rais Samia Suluhu Hassan alionyesha kusikitishwa na kilichotokea Oktoba 29 na kuahidi kuwa hali kama hiyo haitajirudia tena.

Wakizungumza na Pambazuko kwa nyakati tofauti wakazi wa Jiji la Dar es Salaam wamesema tishio la Gen Z limewafanya Polisi kuwajibika kwa nguvu na juhudi tofauti na ilivyozoeleka.

"Maandamano ya hawa vijana yamewafanya Polisi kuonekana wakitenda kazi yao kisawa sawa tofauti na siku za nyuma. Hakika kazi wanayofanya sasa inahalalisha malipo ya mishahara yao," amesema Colin Matebela wa Dar es Salaam.

Naye Mwinjuma Bakalekwa amesema kitendo cha Gen Z kubuni kufanya maandamano kimewaasha askari usingizini kwani pamoja na kuongeza ulinzi ili kudhibiti maandamano hayo, lakini kwa upande mwingine ulinzi huo pia unasaidia kupunguza matukio ya kihalifu.

### Tahadhari ya vurugu

Tahadhari ya kuwepo kwa maandamano hayo kuliwafanya askari Polisi kuzidisha doria wakati wa sherehe za Krismas na mkesha wa mwaka mpya baada ya kuweka ulinzi mkubwa.

Maandamano hayo yaliyoanzia jijini Dar es Salaam na kusambaa katika maeneo mengine ikiwemo Jiji la Arusha, Mwanza, Mbeya, na Dodoma, na maeneo ya mikoa mingine yamesababisha uharibifu mkubwa wa miundo mbinu ya umma na binafsi, ikiwemo vituo vya Polisi, ofisi za umma na za chama tawala - CCM, vituo vya mafuta na maduka kadhaa kuvamiwa, kuporwa na kuchomwa moto.

Kutokana na tishio la maandamano hayo, wanafunzi waliotakiwa kufunga shule Desemba 5 mwaka jana walilazimika kurejeshwa majumbani kabla ya siku hiyo ili kukwepa maandamano ambayo yalipangwa na vijana hao Desemba 9.



Na Rashid MTAGALUKA

Hoja Yangu

# 2026 uwe mwanzo wa mtazamo mpya

KILA mwaka unapowadia, simulizi hubadilika, lakini ujumbe hubaki uleule.

Mwaka mpya huja na hotuba zenye matumaini, kauli nzito za mabadiliko na ahadi zinazovutia masikio ya wananchi.

Viongozi nao hukimbizana kuahidi mageuzi ya kisiasa, ukuaji wa uchumi na kuboreshwa kwa huduma za jamii.

Wananchi pia hutoa maazimio kadhaa ikiwamo kufanya kazi kwa bidii na kushirikiana na serikali.

Lakini, kadri miezi inavyosonga, hali ileile huendelea kujirudia. Mwisho wa mwaka, maswali yaleyale hurudi, je, tulisonga mbele au tulizunguka palepale?

Katika uwanja wa siasa, ahadi zimekuwa sehemu ya ratiba ya kawaida. Kila mwanzo wa mwaka au kipindi cha uchaguzi husikika kauli za "kuongeza ajira kwa vijana," "kupambana na rushwa," na "kuimarisha uwajibikaji." zimekuwa zikijirudia.

Hata hivyo, uhalisia unaonyesha changamoto hizo hizo kuendelea. Takwimu zinaonyesha kuwa zaidi ya asilimia 70 ya nguvu kazi nchini bado ipo katika sekta isiyo rasmi, hali inayowaacha mamilioni bila ajira zenye uhakika, bima ya afya wala hifadhi ya jamii.

Hii inaibua swali kama ahadi zimekuwa suluhisho au ni maneno ya kutuliza matumaini ya wananchi.

Kijamii, Tanzania imekuwa ikijiahidi kila mwaka kujenga jamii yenye maadili, nidhamu na uzalendo. Lakini bado tunashuhudia changamoto zinazojirudia kama rushwa ndogo ndogo, uzembe katika utoaji wa huduma na kudorora kwa mshikamano wa kijamii.

Ripoti za taasisi za udhibiti zinaonyesha kuwa malalamiko mengi ya wananchi yanahusiana na vitendo vya rushwa katika ngazi za chini za huduma.

Hii inaashiria wazi kuwa tatizo si sera pekee, bali ni tabia na utamaduni wa kila siku ambao haujabadilika licha ya ahadi nyingi.

Kiuchumi, licha ya nchi kurekodi ukuaji wa pato la Taifa kwa wastani unaokubalika, maisha ya wananchi wengi bado ni magumu. Takwimu za ustawi wa kaya zinaonyesha kuwa idadi kubwa ya Watanzania hutumia sehemu kubwa ya kipato chao kwa chakula na mahitaji ya msingi, huku gharama za maisha zikiendelea kupanda.

Aidha, ahadi za kupunguza umaskini zimekuwepo kila mwaka, lakini bila mageuzi ya kweli katika uzalishaji, tija na thamani ya kazi, ahadi hizo hubaki kwenye makaratasi na hotuba za viongozi.

Hata hivyo tatizo kubwa si kuwepo kwa ahadi, bali ni ukosefu wa kujifunza kutokana na ahadi zilizopita. Mwaka mpya ungepaswa kuwa nafasi ya tathmini ya kina, nini kilifanikiwa, nini kilishindikana na kwa nini. Bila tathmini, hakuna uwajibikaji; na bila uwajibikaji, ahadi hurudiwa kwa urahisi bila hofu ya kuulizwa.

Mwaka mpya basi usiwe mwanzo wa ahadi mpya tu, bali uwe mwanzo wa mtazamo mpya. Mtazamo unaowapima viongozi kwa matokeo, si maneno; unaowafanya wananchi kuuliza maswali yenye ushahidi; na unaolazimisha taasisi kujifunza badala ya kurudia kauli zilezile.

Kwa maana, taifa lisilojifunza kutokana na ahadi zake za jana, hulazimika kuziimba tena kesho, kwa sauti ile ile, bila mabadiliko ya kweli.

***Rashid Mtagaluka ni mwandishi wa habari na anapatikana kwa simu nambari 0784 438 546 na email; mtagaluka@gmail.com***



# Wengi walia ukata wa Januari

Na Mwandishi WETU

NDIYO kwanza mwaka wa 2026 bado mbichi.
Kama kawaida, "vilio" vya ukata wa Januari bado vinasikika kutoka kwa idadi kubwa ya Watanzania; wengi wanadai maisha yamekuwa magumu kwa kuwa hakuna ajira, hivyo mzunguko wa fedha kuwa mdogo na kuwagusa wachache.

Hata hivyo, vilio vya Januari, vimekuwepo kila mwaka. Hakuna mwaka unaoanza bila kuwepo kwa "maumivu" haya. Sasa imekuwa mazoea.

Hii inatokana na kuwepo kwa matumizi makubwa na mengi wakati wa mwisho wa kila mwaka na mwanzo wa mwaka.

Katika kipindi hiki kuna matumizi ya lazima ikiwamo ada za shule ama vyuo na kodi za nyumba.

Lakini msingi wa tatizo ni tabia ambayo watu wengi wanayo - kutojiandaa kwa ajili ya matumizi hayo ambayo yanajulikana na kila familia.

Hali hii inawalazimisha watu wengi "kukuna vichwa" na kuwaza namna ya kuendesha maisha, hasa katika mwezi huu wa Januari.

Pamoja na ulazima wa matumizi ya fedha kwa mwisho wa mwaka, pia wapo watu wanaoamua kutapanya fedha Desemba kutokana na kuwa na heka heka nyingi za shughuli za sherehe za mwisho wa mwaka kama Krismas na mwaka mpya.

Shughuli hizo zinazohitaji matumizi makubwa ya fedha ikiwamo maandalizi. Ni katika kipindi hicho, familia nyingi "hujiachia" kwa kula na kunywa vyema zaidi, kusafiri wakati wa likizo na wengine kutembelea maeneo ya vivutio.

Hali ya ugumu wa maisha katika kipindi hiki cha mwanzo wa mwaka haiwaathiri wananchi wa kawaida pekee, bali hata wafanyabiashara kama ambavyo ufuatiliaji uliofanywa na Pambazuko katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es salaam ulivyothibitisha.

Katika mahojiano, wafanyabiashara kadhaa wamekiri kuwa nao wanakabiliwa na hali ngumu kwa sababu idadi ya wateja imepungua sana kutokana na watu kubana matumizi.

"Watu kukosa fedha katika mwezi huu wa Januari, kunatuathiri hata sisi wafanyabiashara. Tuna hali ngumu kwa sababu biashara zetu zinategemea hao watu ambao hivi sasa wanalalamika ukata," anasema Peter Chigwala, mfanyabiashara wa bucha la nyama katika eneo la Vingunguti Dar es Salaam.

Chigwala anabainisha kuwa mauzo ya nyama kwa kipindi hiki yameshuka kwani watu wanabana matumizi na kuona kitoweo hicho kama anasa.

Anasema kabla ya Januari alikuwa akiuza hadi kilo 100 za nyama kwa siku, lakini hivi sasa anauza kati ya kilo 25 hadi 30 tu kwa siku.

Naye muuza nyama mwingine kwenye bucha katika eneo la Kijichi, Temeke, Dar es Salaam, Salumu Yusuf, amesema biashara imekuwa ngumu kipindi hiki. Amesema kutokana na hali ngumu ya mwanzo wa mwaka hivi sasa huuza kilo 30 au zaidi kidogo za nyama kwa siku tofauti na kipindi cha kawaida.

"Kipindi hiki tunakijua ni nadra kuuza kwa kiwango tulichozoea. Kwa mfano mimi huwa nauza kilogramu 60 za nyama kwa siku kipindi cha kawaida lakini sasa imekuwa tofauti,"anasema Salum. Mfanyabiashara wa genge eneo hilo, anayeuza kwa jumla na reja reja, Upendo Samweli, amesema kwake biashara imekuwa ngumu kutokana na wateja kununua vitu kwa uchache.

"Hali imebadilika sasa hivi mteja anakuja na kutaka kitu kimoja kimoja mfano kitunguu, nyanya au viazi vya bei ndogo wakati miezi ya kawaida ambayo wateja walikuwa wakinunua vitu kwa wingi na kwa siku najikuta nikiuza shilingi 80,000 na kuendelea," amesema Upendo.

Mfanyabiashara wa bajaji, John Lyimo, amesema biashara ya usafirishaji nayo imekuwa ngumu.

"Kazi ni ngumu kwa sababu watu wengi sasa wameacha kupanda boda na bajaji na wamerudi kwenye daladala. Kwa mfano kabla ya mwezi Januari asubuhi nilikuwa nachukua abiria mmoja mmoja kwa bei ya shilingi 3,000 kwenda Kivukoni vivyo hivyo kwa jioni lakini hivi sasa tunaunga unga tu," amesema John. Muuza duka la vyakula eneo la Tandika, Temeke Jackson Mwambogo, amesema hali ya maisha kwa Januari imeshusha mauzo ya bidhaa zake.

Ameeleza zamani kwa siku alikuwa akiuza kilo 500 za mchele lakini kwa sasa huuza kilo 300 hadi 200, maharagwe alikuwa akiuza kilo 80 lakini kwa sasa anauza ni 34 wakati unga anauza kilo 70 tu badala ta zaidi ya kilo 100 alizokuwa akiuza awali.

# Habari katika picha




*Mkurugenzi wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Dkt. Peter Kisenge, akionyesha bango la huduma za matibabu ya kibingwa kwa raia wa kigeni kutoka nchi mbalimbali duniani baada ya kuzinduliwa katika tawi la JKCI Oysterbay, Dar es Salaam hivi karibuni. (Na Mpigapicha Wetu)*



*Wafanyabiashara ya samaki katika soko la Feri wakiuzia samaki akina mama kwa ajili ya kwenda kuwauzia wateja huko mitaani, Dar es Salaam jana. (Na Mpigapicha Wetu)*




*Magari ya vikosi vya zimamoto yakiwa yamezingira jengo la NSSF lililopo mtaa wa Azikiwe na Samora baada ya kutokea ajali ya moto ambao uliweza kudhibitiwa kabla haujaleta madhara zaidi jijini Dar es Salaam juzi. (Na Mpigapicha Wetu)*

■ Utalii

# Maajabu ya mchanga 'unaotembea' Hifadhi ya Ngorongoro



Na Mwandishi WETU

WASWAHILI husema tembea uone na mwenda bure siyo sawa na mkaa bure, huenda ataokota.

Ukitaka kuona mchanga unaohama – au unaotajwa kutembea, nenda jirani na Bonde la Olduvai ndani ya Hifadhi ya Ngorongoro uamini.

Haya ni maajabu mengine yanayopatikana kwenye hifadhi hiyo ya kipekee Afrika na duniani.

Mtalii yeyote wa ndani ama wa nje akipanga safari ya kwenda Ngorongoro, basi asitarajie kuona wanyamapori tu.

Ukipata nafasi, basi fika eneo la mashariki la uwanda wa Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, karibu na Olduvai Gorge ndani ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro.

Ni katika eneo hilo, ambako utastaajabu kuona maajabu ya matuta makubwa ya mchanga unaohama.

Mchanga huu huhama kwa mita 15 hadi 29 kwa mwaka bila kubadili umbo lake la mwezi mchanga ukiwa umejikusanya pamoja bila kuacha mabaki nyuma.

Mchanga huo hupeperushwa na mawimbi ya upepo kuelekea eneo la magharibi hadi kuvuka eneo la tambarare.

Tukio hili ni mojawapo ya mambo ya kuvutia na kukuacha kinywa wazi uwapo ndani na eneo la Ngorongoro.

Wataalamu wanasema mchanga huu wenye rangi nyeusi umetokana na madini ya chuma na majivu yaliyotokana na mlipuko wa Volcano kutoka Mlima Oldoinyo Lengai.

Mchanga huu ambao husogea kwa kasi ya takribani mita 15–29 kwa mwaka, tuta lake lina urefu wa mita tano na upana wa mita 100.

Kuhama hama huku kumesafisha sehemu nyepesi za majivu kutoka eneo hilo, na kuacha nyuma madini ya chuma yenye rangi nyeusi ambayo yaliunda mchanga huo.

Unaweza usihisi kuwa mchanga huo hauendi sehemu yoyote, kwani huhama kwa njia ya mtiririko kwa kasi ndogo na hivyo kuchukua muda mrefu kusogea kutoka eneo moja hadi jingine.


Utagundua uhamaji wake kutokana na alama za mawe zilizowekwa eneo hilo, zikionesha mahali mchanga ulipo kwa wakati huo, na wapi ulikuwepo hapo kabla.

Mchanga huo hujumuisha majivu ya volkano, yenye nguvu ya sumaku, yenye uwezo wa kushikilia chembechembe za mchanga huo pamoja.

Wageni wanaofika eneo hili, hustaajabu sumaku ya mchanga huu ukinatisha simu zao za mikononi, na hata vitu vingine vyenye asili ya chuma.

Hayo ndiyo maajabu ya Hifadhi ya Ngorongoro ukitaka kujua zaidi kuhusu mchanga huu tembea uone kwani fahari ya macho ni kuona na fahari ya macho haifilisi duka.

# Soma vitabu




Je, wewe unapenda kujifunza na kupata uelewa wa mambo anuani?

Kama jibu ni ndiyo, basi kuwa tayari kupata nakala yako ya vitabu vifuatavyo kutoka kwa mwandishi Simon Martha Mkina;

1. Mwalimu Nyerere Hazina Tanzania

- Kitabu hiki kilichapishwa mara ya kwanza 1999 mara baada ya kufariki kwa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Sasa kinachapishwa kwa kurejerewa na kuwemo kwa mambo kadhaa ambayo hayakuwahi kuwemo kwenye kitabu cha awali.

2. Ink meets Mic meets Camera: A Journalism Primer

- Kitabu hiki kinachapishwa kwa mara ya kwanza ikiwa ni mwongozo wa mafunzo kwa waandishi wa habari wapya na hata wale wanaotaka kujifunza zaidi kuhusu umahiri katika uandishi wa habari wa magazeti, redio, blog, televisheni (ikiwamo zile zinazotangaza mitandaoni).

Nini kifanyike: Ikiwa utapenda kupata nakala ya vitabu hivi - au kimoja wapo, unatakiwa kuandika ujumbe mfupi kwenye simu yako na kutuma kwa namba hii: 0754 020880. Taja kitabu unachopenda kukipata mara baada ya kuanza kuuzwa. Vitabu hivi vitauzwa kwa njia ya upekee kwa wale wanaoandika ujumbe kwanza kabla ya kuanza kuuzwa kwenye maduka ya vitabu Tanzania nzima. Bei ya kitabu kuhusu Mwalimu Nyerere ni Shilingi 20,000 na kile cha mafunzo ya uandishi wa habari ni Shilingi 30, 000.

Karibuni sana tuendelee kujifunza.

Elimu ni bahari!

Na Anti MSHAURI





# Uhusiano mzuri ni tiba

KARIBU msomaji wangu wa safu ya uhusiano uweze kujipatia maarifa mbalimbali kuhusiana na masuala ya maisha.

Ni matarajio yangu kuwa umeuanza mwaka salama.

Leo nitazungumza uhusiano unavyoweza kuboresha maisha.

Uhusiano ni jambo muhimu katika maisha kwani bila uhusiano mzuri maisha yanakuwa magumu.

Uhusiano unaweza kuwa wa aina mbalimbali; kama vile wa kifamilia, urafiki, mapenzi, kikazi, na hata ya kijamii.

Uhusiano hutoa msaada wa kihisia na kisaikolojia hasa kwa mtu anayepitia changamoto nyingi kimaisha.

Uhusiano mzuri unaweza kupunguza msongo wa mawazo, huzuni, na hofu kwa sababu mtu ana nafasi ya kushiriki hisia zake na kupokea faraja.

Uhusiano huimarisha furaha, huleta utulivu wa moyo ikiwa mlengwa atajijengea misingi ya kuwa karibu na watakaompatia furaha hiyo.

Mfano katika ndoa; mume na mke wanaweza kuuimarisha vyema uhusiano wao ikiwa watauenzi na kuudumisha uhusiano wao katika nyanja zote za kuyaishi maisha ya ndoa kwa upendo na kuvumiliana.

Uhusiano kikazi unaweza kudumishwa ikiwa kuna maelewano mazuri kati ya wafanyakazi lakini pia kufanya kazi kwa ushirika vivyo hivyo kwa familia na katika nyanja nyingine.

Uhusiano huongeza mafanikio na maendeleo katika maisha, na hakuna mtu anayeweza kufanikisha kila kitu peke yake na kupitia mahusiano, watu hupata msaada wa kiakili, kifedha, na hata kimkakati.

Uhusiano kibiashara unaweza kumsaidia mtu kupanda ngazi na kufanikisha malengo yake kwa urahisi zaidi.

Kikubwa na kitu cha msingi kufanikisha uhusiano mzuri ni kwa watu wa makundi tofauti kuishi kwa kushirikiana kikamilifu.

***Kwa maoni na ushauri: hellen2ngoromera@gmail.com Au simu: 0715 88 67 49.***



# ‘Transformative Teal;’ rangi ya mwaka 2026

RANGI ya mwaka 2026 kulingana na sayansi ya rangi imetangazwa kuwa ni Transformative Teal.


Ili mambo yasiwe mengi unaweza kuita ‘teal green’ au ‘crystal green.’

Rangi hii ina mvuto wa kipekee ambayo inawapendeza watu wa rangi zote.

Kwa mujibu wa falsafa ya Feng Shui, Transformative Teal inaunganisha vipengele vya maji na miti.

Rangi hii inaweza kutumika kupitia mapambo ya kuta, vifaa vya ndani ya nyumba au ofisini, pamoja na vitambaa.

Zaidi ya kuwa mtindo wa rangi, Transformative Teal ni ujumbe unaokumbusha umuhimu wa kubadilika kwa malengo yaliyo wazi huku tukibaki na utulivu wa ndani katika safari ya maisha.



# Jali ngozi yako kwa urembo wa asili

UZURI wa ngozi siyo rangi tu, bali ni muonekano wa ngozi inayong’aa ambayo inaashiria afya njema.

Utunzaji wa ngozi siyo lazima kutumia vipodozi vya gharama kubwa, unaweza kuandaa mwenyewe ukiwa nyumbani kwako.

Kwa mfano; unapofanya treatment ya uso wako unaweza kutumia kiini cha yai, machicha ya nazi, tango na limao.

Pia ni muhimu zaidi kula matunda kwa wingi kama machungwa, matikiti, tango pamoja na mboga za majani.



# Ray C akumbuka nyumbani, lakini...



**Na Mwandishi WETU**

MWANAMUZIKI wa zamani wa muziki wa Bongo Fleva, Rehema Chalamila almaarufu Ray C, amesema anatamani kurudi nyumbani Tanzania, lakini kuna vitu akivifikiria anaona ni bora aliondoka.

Ray C, ambaye kwa sasa anaishi jijini Paris, Ufaransa ameandika ujumbe huo kwenye ukurasa wake wa mtandao wa Instagram.

"Kuna muda na-miss nyumbani, lakini kuna muda naona bora nilivyojiondokea," ameandika Ray C.

Ujumbe huo wa Ray C, unaonyesha kuwa ni wazi amekumbuka kuyaishi maisha ya nyumbani.

# Davido ampa onyo mwanamke aliyedai kuzaa naye

**Na Mwandishi WETU**

MSANII wa muziki kutoka Nigeria, David Adedeji Adeleke almaarufu Davido, ameweka wazi msimamo wake baada ya vipimo vya DNA kuonyesha kuwa yeye siyo baba wa mtoto wa binti anayejitambulisha kuwa amezaa naye.

Amemtaka binti huyo atafute baba wa mtoto huyo.

Kupitia ukurasa wake wa mtando wa X, Davido amesema walikubaliana kuchagua hospitali kwa pande zote mbili, ambapo yeye alichagua hospitali tatu, huku upande wa pili ukichagua hospitali mbili.

Vipimo hivyo ambayo vilifanyika katika hospitali tano zote vilionyesha kuwa binti huyo siyo mtoto wake.

"Vipimo vyote vilitoka 'negative'. Hii ndiyo mara ya mwisho nitaongea kuhusu upuuzi huu," aliandika Davido.

Ameongeza kuwa hakuwahi kuwa na uhusiano na mama wa mtoto huyo, akisema walikutana tu wakati wa taratibu za vipimo vya DNA.

Binti huyo anayejitambulisha kuwa ni Anuoluwapo Adeleke, amesema amepata maumivu ya kihisia baada ya majibu ya DNA.

Kwa mujibu wa binti huyo, madai ya Davido kwamba kulikuwa na vipimo vitano vya DNA yanapingwa vikali na upande wake.

Amesema kwa mujibu wa maelezo ya mama yake, kulifanyika kipimo kimoja tu, ambacho anadai hakikuwa halali, akielekeza umma kusoma taarifa ya mama yake iliyowekwa juu ya ukurasa wake.

# Jinsi ya kusoma Pambazuko






# Iliyovuna Tanzania Afcon

Na Mwandishi WETU

KATIKA michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon), Tanzania kwa mara ya kwanza iliweza kupenya na kuingia kwenye kundi la timu 16 bora.

Hatua hii ndiyo ilikuwa mara ya kwanza kwa Tanzania kuifikia tangu kuanza kwa michuano hiyo mikubwa zaidi Afrika.

Pamoja na kwamba haikuendelea kwenye hatua zilizofuata, lakini kuna mengi wachezaji wa timu ya taifa; Taifa Stars wamejifunza.



Tanzania iliposhiriki katika mashindano haya, ilipata fursa ya pekee ya kujifunza na kuboresha soka lake.

Moja ya mambo makuu ambayo Tanzania imejifunza ni umuhimu wa maandalizi ya kina.

Katika michuano hiyo, Taifa Stars, ilidhihirisha ukweli kwamba maandalizi mazuri ni muhimu katika kufanikisha matokeo chanya.

Katika mashindano ya Afcon, ushindani ni mkali, hivyo ushirikiano wa timu, mipango sahihi, na mazoezi ya mara kwa mara ni muhimu sana. Hii inasisitiza haja ya Tanzania kuwekeza zaidi katika mazingira bora ya mazoezi na vifaa ili kukuza ufanisi wa wachezaji.

Pili, mashindano haya yameonyesha umuhimu wa uajiri wa wakufunzi wenye ujuzi. Kwa kupitia mechi nyingi na uzoefu walioupata kutoka kwa makocha wa timu nyingine, Taifa Stars inahitaji kuongeza maarifa na mbinu sahihi za kikosi chao. Kuajiri makocha wenye uzoefu wa kimataifa kutasaidia kuongeza ubora na ufanisi wa timu katika mashindano yajayo.

Aidha, ushirikiano kati ya vyama vya soka na wadau mbalimbali ni muhimu. Tanzania imeweza kuona jinsi Afrika, hasa katika nchi kama Senegal na Ghana, wanavyomiliki mifumo bora ya ukuzaji wa soka.

Ushirikiano wa serikali, kampuni, na mashirika yasiyo ya kiserikali, inaweza kusaidia katika kukuza mifumo ambayo itawasaidia wachezaji na makocha kwa pamoja.

Pia, mashindano ya Afcon yameleta uelewa muhimu kuhusu umuhimu wa maendeleo ya vijana. Tanzania inahitaji kujikita zaidi katika kuwawezesha vijana kupitia ligi za vijana na programu za ukuzaji wa talanta.

Hii itachangia kupata wachezaji wenye ubora wa juu ambao wanaweza kuwa nguzo muhimu katika timu ya Taifa siku zijazo.

Kwa kumalizia, mashindano ya Afcon hapo jana kumeleta mafunzo muhimu kwa soka la Tanzania. Kwa kuzingatia maandalizi, uajiri wa wakufunzi bora, ushirikiano na wadau, na maendeleo ya vijana, soka la Tanzania linaweza kupata mafanikio zaidi katika siku zijazo.

Ikiwa mashirika na wahusika wote watafanya kazi kwa pamoja, Taifa Stars inaweza kufanikiwa na kurudi katika ramani ya soka Afrika na kuwa bora zaidi kwenye michuano ijayo ambayo itafanyika Mafrika Mashariki; Kenya, Uganda na Tanzania mwaka 2027.

*GAZETI hili lilianzishwa 2021, kuandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaendeshwa kwa ushirikiano wa mzunguko – kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.*

TAMPA
TANZANIA MEDIA PRACTITIONERS ASSOCIATION